tigo pesa SportPesa
MAOKOTO Deilee!
WEKA ZAIDI,BET USHINDE ZAIDI
SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#

Jumanne Oktoba 10, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581459 www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



# Mjema: Samia urais hadi 2035

• **Asema** ngwe miaka 10 inaanza 2025, wadau waibuka...*Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

### WATALII WAENDELEA KUMIMINIKA NCHINI

KATIKA kipindi cha kuanzia Januari hadi Agosti, 2023 idadi ya watalii...



UKURASA WA 3

### 11 MBARONI TUHUMA DAWA ZA KULEVYA



WATU 11 wamekamatwa kwa tuhuma za kulima na kusafirisha...

UKURASA WA 19

### SHULE ZAFUNGWA UFARANSA KUTOKANA NA KUNGUNI

WAZIRI wa Elimu wa Ufaransa, Gabriel Attal, amesema kuwa nchi...



### Watanzania hawajulikani mahali waliko

UKURASA 19



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Waziri Mkuu wa India, Narendra Modi, baada ya mkutano na waandishi wa habari uliofanyika New Delhi, India jana. **PICHA: IKULU**

**MAENEO YA MAKUBALIANO**

- Kujenga uwezo, mafunzo katika ulinzi na usalama
- Matumizi ya Shilingi na Rupia katika biashara.
- Ushirikiano katika sekta ya uchukuzi
- Uwekezaji katika miradi ya maendeleo
- Kuendeleza utamaduni na michezo
- Teknolojia ya habari na mawasiliano
- Maendeleo ya sekta ya afya

# Tanzania, India zakubaliana kuimarisha maeneo kimkakati

UKURASA 3

**MICHEZO** NYOTA YANGA SASA KUWANIA MAMILIONI UK.24 **KATUNI** UK.6

# Mjema: Samia urais hadi 2035

**Na Christina Mwakangale**

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Sophia Mjema, amesema kutokana na kile anachoendelea kukionyesha Rais Samia Suluhu Hassan kwa Watanzania, ni wazi kwamba anastahili kupewa miaka 10 kuanzia mwaka 2025.

Kwa mantiki hiyo, kutokana na kauli ya Mjema, Rais Samia kipindi chake cha uongozi wa nchi kinapaswa kufikia ukomo mwaka 2035.

Amesema Rais Samia anastahili kupewa miaka 10 kwa kupigiwa kura kwa kuwa amethibitisha kuwa mwanamke akipewa nafasi yoyote ya uongozi, ikiwamo kuongoza nchi, anafanya vyema.

Wakati Mjema akitoa kauli hiyo, wanasiasa na wadau wametoa maoni yao wakisisitiza kuwa nchi inaongozwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ambayo ndiyo imemweka Rais madarakani. Wanasheria nao wamesema kauli hiyo ya Mjema inawezekana tu iwapo katiba itabadilishwa.

Mjema aliyasema hayo jana alipozungumza na wanawake wa mkoani Mara. Alisema sasa wanawake wanapewa jukumu kubwa la kufanya kweli na kutimiza jambo lao mwaka 2024 na 2025 (miaka ya uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu wa Rais, wabunge na madiwani).

"Tunaye kiongozi wetu Rais Samia Suluhu Hassan ambaye kwa kweli ameonyesha kitu cha tofauti. Haijapata kutokea watu walifikiria kwa kipindi hiki kifupi ambacho tutampa mwanamke, anaweza asiweze. Jamani si mmeona mambo hayo na muziki wake, miradi, fedha.

"Mwenyezi Mungu ameweka mkono wake akampa ujasiri akaunganisha zile nguvu zake awe na maono. Mungu akiunganisha nguvu hizo wanadamu wanaweza? Sisi wanawake tupo tuhakikishe tunamuunga mkono. Sasa hivi wanawake heshima iliyopo ndiyo kwanza anaanzia pale mwaka 2025. Tunaanza kumpigia kura. Tumeona kazi zake, ametudhihirishia kuwa kazi hii anaiweza bila tatizo lolote... acha waseme," alisema.

Alisema utaratibu uliopo ni kiongozi anayewania nafasi ya urais kipindi chake ni miaka 10, yaani mihula miwili, kila mmoja ukiwa na miaka mitano.

"Wanawake mwaka 2025 ndio tunaanza, wanawake mmenielewa. Anaanza mwaka 2025 na anamaliza 2035, katufanyia kazi nzuri. Hivi akisimama mwanamke mwenzio pale kafanya vizuri, unajisikiaje? Hata wakiwa wote wanawake hakuna ubaya, maadamu wanafanya kazi sawa.

"Leo kafanya vizuri, ikija miaka mingine tunasema ndiyo, mingine tena ndiyo kwani kuna ubaya? rais mwanamke, makamu wa rais mwanamke, waziri mkuu mwanamke, Spika mwanamke," alisema.

Mjema alisema Rais Samia aendelee kuungwa mkono, kutokana na kazi anayoendelea kuifanya na kuwahakikishia Watanzania kwamba anaweza jukumu lake la urais.

"Tunataka Tanzania tufike 50/50 kwenye uongozi na uamuzi serikalini ndiyo tunamwona Rais anachokifanya. Mimi kama mwenezi wa kwanza mwanamke niko kule juu," alisisitiza.

**WADAU WAIBUKA**

katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, ametoa maoni kuhusu kauli hiyo akisema awamu aliyopo Rais sasa mamlakani ni kamili na muhula wake utakamilika 2025, huku wa pili ukitarajiwa kukamilika mwaka 2030.

"Sisi tunachofahamu hii ni awamu mpya. Awamu ya sita inaanza pale Rais amechukua madaraka na kuendelea bila kujali kwamba alipochukua ilikuwa mwaka mmoja umeanza kutumika. Mwaka 2025 hadi 2030 ndicho kipande cha pili cha awamu ya sita, hii ni awamu kamili," alisema.

Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mrema, alisema: "Rais Samia ni zao la katiba, hivyo katiba inapaswa kuzingatiwa kuhusu ukomo wa madaraka wa Rais kama ilivyoainishwa.

"Mwaka 1985 wakati Mwalimu (Julius) Nyerere anang'atuka, aliwahi kusema wako watu walimwambia Mwalimu ukiondoka nchi itayumba, unamwachia nani nchi. Mwalimu aliwakemea akawaambia wao matumbo yao ndio yatayumba. Rais Samia awakemee wanaomtaka watu wanaotoa kauli hizi kwa sababu hawamtakii mema."

Naye Naibu Katibu Mkuu Chama cha Wananchi (CUF), Magdalena Sakaya, alisema katiba iliyopo inatoa mwongozo kwamba Rais anapoingia madarakani, anaingia na mamlaka kamili na si kumshikia mamlaka aliyekuwapo awali.

"Kwa katiba yetu, Rais anaongoza kwa vipindi viwili. Kaanzia miaka mitano alipoikuta na atamaliza miaka mingine hadi 2030," alisema.

**LHRC YAFAFANUA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Shreria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, alisema katiba imeeleza kuhusu rais kuwapo madarakani kwamba iwapo itafanyika hivyo, kwa mujibu wa Mjema, itamaanisha Rais aliyeko mamlakani ataongoza kwa miaka 14.

"Anaweza kwa miaka mitano tu...Rais (John Magufuli) angekuwa amefariki dunia chini ya miaka minne, angeweza kuchaguliwa vipindi viwili lakini kwa sasa labda kama katiba itabadilika," alisema.

Aliongeza kuwa: "Katiba inasema endapo Makamu wa Rais anashika kiti cha Rais kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 37(5) kwa kipindi kinachopungua miaka mitatu, ataruhusiwa kugombea nafasi ya urais mara mbili, lakini kama akishika kiti cha urais kwa muda wa miaka mitatu au zaidi ataruhusiwa kugombea nafasi ya urais mara moja tu."



Mwongoza watalii kutoka Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), Omary Sharif, akitoa ufafanuzi kwa wafanyakazi wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) kuhusu aina ya vivutio vilivyopo ndani ya Msitu wa Mazingira Asilia Pugu Kazimzumbwi uliopo Kisarawe mkoani Pwani mwishoni mwa wiki iliyopita. **PICHA: JKCI**

## Watalii waendelea kumiminika nchini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA kipindi cha kuanzia Januari hadi Agosti, 2023 idadi ya watalii walioingia nchini imeongezeka na kufikia 1,131,286 ikilinganishwa na 900,182 walioingia nchini kipindi hicho mwaka jana.

Sababu ya ongezeko hilo zimetajwa kuwa ni uzinduzi wa Filamu ya The Royal Tour nchini Marekani iliyoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan na Tanzania kuwa na vivutio vingi ikilinganishwa na mataifa mengine duniani.

Mkurugenzi wa takwimu za uchumi Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Daniel Masolwa, alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ongezeko la watalii walioingia nchini katika pindi hicho.

Alisema kuna ongezeko la watalii 231,104 sawa na asilimia 25.7 na kati ya hao wote walioingia nchini katika kipindi hicho 236,047 walipitia Zanzibar sawa na asilimia 31.1.

"Ofisi ya Taifa ya Takwimu inajukumu la kusambaza takwimu za kijamii na kiuchumi kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu sura 351 miongoni mwa taarifa hizo ni takwimu za mara kwa mara za mwenendo wa watalii walioingia nchini," alisema Masolwa.

Kadhalika, alisema watalii walioingia nchini katika kipindi cha mwezi Agosti 2023, waliongezeka hadi 186,030 ikilinganishwa na 158,049 mwezi Agosti, mwaka jana sawa na ongezeko la asilimia 17.7.

"Watalii 336,203 kati ya wote walioingia nchini mwezi Agosti, 2023 kupitia Zanzibar sawa na asilimia 29.7 na idadi ya watalii wote," alisema Masolwa.

Alisema idadi hiyo ya walongia nchini kutoka nchi zilizo nje ya Bara la Afrika katika kipindi cha Januari hadi Agosti mwaka huu ni Marekani ikiwa na jumla ya watalii 84,541.

"Mtakumbuka Filamu ya Royal Tour ilizinduliwa kwa mara ya kwanza nchini Marekani hii inaonyesha kuwa juhudi zile za Rais Samia Suluhu Hassan zimelipa kutokana na ongezeko hili," alisema.

Pia alisema mataifa mengine yaliyoleta watalii wengi nchini nyuma ya Marekani ni Ufaransa (72,009), Ujerumani (57,798), Uingereza (51,056) na Italia (51,056).

"Aidha, mwezi Agosti 2023 pekee idadi ya watalii walioingia nchini walitoka Italia (14,986), Marekani (14,416), Ufaransa (11,997), Uingereza (9,852) na Ujerumani (9,161)," alisema.

Vilevile, alisema katika kipindi cha Januari hadi Agosti, Tanzania ilipokea watalii kutoka Bara la Afrika na wengi wao walitoka katika nchi ya Kenya (128,753), Burundi (69,505), Zambia (38,394), Rwanda (37,269) na Uganda (4,052).

Alisema, sekta ya utalii ni miongoni mwa vyanzo vikuu vya fedha za kigeni nchini na kwamba taasisi na kampuni zinazotoa huduma kwa watalii zinatakiwa kuendelea kutoa huduma bora zaidi kwa lengo la kuwavutia wapya na waliokuja waje kwa mara nyingine.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
07.10.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **10.10.2023** hadi **17.10.2023** kampuni ya **CEVA Interfreight** itasafirisha magari matupu wenye vipimo vikubwa kutoka **Mzenga kuelekea Bandari ya Dar Es Salaam,** gari hilo lenye namba za usajili **NRB97300 / NRB54202 DS00TGGP / NRB53910**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **Mita** | **36.5** |
| **Upana** | - | **Mita** | **4.30** |
| **Kimo** | - | **Mita** | **4.60** |

3. Njia itakayotumika: **Mzenga hadi Bandari ya Dar Es Salaam** kupitia **Barabara ya Morogoro, Barabara ya Mandela** gari litasafiri muda wa mchana ***( Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

117638302

# Tanzania, India zakubaliana kuimarisha maeneo kimkakati

**Na Jenifer Gilla**

TANZANIA na India zimekubaliana kuimarisha ushirikiano kwenye maeneo ya kimkakati kwa manufaa ya pande zote yakiwamo maji, kilimo, teknolojia, afya, ulinzi na usalama, utamaduni na michezo, uchukuzi, biashara na uwekezaji.

Nchi hizo pia zimetiliana saini hati 14 za makubaliano na mkataba mmoja. Hati 10 zimehusisha taasisi za serikali na tano ni za sekta binafsi.

Hayo yalibainishwa jana wakati wa mkutano wa pamoja kati ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu wa India, Narendra Modi na waandishi wa habari uliofanyika katika jengo la kupokelea wageni wa kitaifa la Hyderabad House, jijini New Delhi.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Rais Samia aliipongeza serikali ya India kwa kuendelea kuwa mshirika muhimu na kuchangia maendeleo ya Tanzania hususan kwenye maeneo ya kimkakati.

Pia alisema Tanzania inapongeza uamuzi wa serikali hiyo kuanzisha tawi la kwanza la Taasisi ya Teknolojia ya India nje visiwani Zanzibar. Alisema uamuzi huo ni heshima na upendeleo kwa Tanzania kwa kuwa utawanufaisha Watanzania na Afrika Mashariki na Kati kwa ujumla.

Rais Samia alisema ushirikiano wa nchi hizo umeongeza thamani ya ufanyaji biashara na takwimu zinaonyesha kuwa biashara imeongezeka hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 3.1 mwaka 2022 kutoka Dola za Marekani bilioni 2.6 mwaka 2017.

Rais Samia pia alimpongeza Waziri Mkuu Modi kwa kuandaa kwa mafanikio Mkutano wa Wakuu wa Nchi za G20 uliofanyika nchini humo Septemba, mwaka huu na kuipongeza India kwa kuitetea Afrika kupitia Umoja wa Afrika kuwa mwanachama wa kudumu wa umoja huo.

"Siwezi kusita kuipongeza India kwa kufanikiwa kuandaa Mkutano wa G20. Waziri Mkuu Modi ameitetea Afrika kuwa mwanachama kamili wa G20. Ametetea mpango wa kupunguza madeni kwa mataifa madogo na kutangaza mpango wa dharura wa kuhamasisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya nchi zinazoendelea ili kuwezesha upatikanaji wa teknolojia ya nishati safi ifikapo mwaka 2050," alisema.

Waziri Mkuu Modi aliitaja Tanzania kuwa mshirika wake wa karibu na mkubwa katika maendeleo barani Afrika na Tanzania na India zimekubaliana kukuza ushirikiano uliopo katika viwango vya juu vitakavyowanufaisha wananchi wa mataifa hayo.



Alisema India itaendelea kushirikiana na Tanzania kwenye maeneo mbalimbali, yakiwamo kukuza ujuzi, usambazaji maji, teknolojia ya habari na mawasiliano, uhusiano wa watu wa India na Tanzania, nishati safi, ulinzi na usalama.

Pia alisema nchi hizo zimekubaliana kuwa na mpango wa miaka mitano ya ushirikiano katika masuala ya ulinzi na usalama hususan katika maeneo ya kujenga uwezo, mafunzo na ulinzi baharini.

Kuhusu ushirikiano katika biashara, Waziri Mkuu huyo alisema nchi hizo zimekubaliana kutumia sarafu za nchi zao kukuza na kuongeza biashara baina ya nchi hizo pamoja na kupunguza gharama na matumizi ya Dola za Marekani.

Wakati wa mkutano huo, wakuu hao walishuhudia ubadilishanaji wa hati sita za makubaliano ya ushirikiano baina ya mataifa yao katika sekta za uchukuzi, utamaduni, michezo, uwekezaji, TEHAMA na afya.

Baadhi ya hati hizo ni makubaliano kati ya Wizara ya Elektroniki na Teknolojia ya Habari ya India na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ya Tanzania kuhusu ushirikiano wa kupeana suluhu zenye mafanikio za kidijitali zinazotekelezwa kwa ujuzi wa idadi ya watu kwa ajili ya mabadiliko ya kidijitali.

Nyingine mabadilishano ya hati ya makubaliano ya kiufundi kati ya Jeshi la Wanamaji la India na Shirika la Wakala wa Meli wa Tanzania (TASAC) kuhusu kupeana taarifa za meli za kibiashara.

Nchi hizo pia zilitia saini makubaliano ya mpango wa kubadilishana utamaduni kati ya India na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miaka ya 2023 hadi 2026.

Zingine ni makubaliano kati ya Baraza la Michezo la Taifa la Tanzania na Mamlaka ya Michezo ya India kuhusu Ushirikiano katika Sekta ya Michezo na Hati ya makubaliano kati ya Coaching Shipyard Limited na Marine Services Corporation Limited kuhusu ushirikiano katika sekta ya bahari.

Pia hati ya makubaliano kati ya Mamlaka ya Bandari ya Jawaharlal Nehru chini ya Wizara ya Usafirishaji wa Bandari na Njia za Majini ya India na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kwa ajili ya kuanzisha bustani ya viwanda nchini Tanzania.

Kamishna wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) chini ya Wizara ya Fedha, David Kafulila, alisema kupitia ziara hiyo atakwenda kujifunza mambo mengi hasa namna nchi hiyo ilivyojikomboa kiuchumi.

Alisema miaka michache iliyopita India ilikuwa na uchumi wa chini kama zilivyo nchi nyingi zinazoendelea, lakini umekua na inakadiriwa baada ya miaka mitano ijayo itakuwa nchi ya tatu kwa ukubwa wa uchumi duniani.

Alisema kwa kipindi cha miaka 10, biashara kati ya nchi hizo mbili imefikia zaidi ya dola bilioni 24 ambayo takribani asilimia 30 ya uchumi wa Tanzania..

## Watu 11 mbaroni tuhuma kukutwa dawa za kulevya

**Na Gwamaka Alipipi**

WATU 11 wamekamatwa kwa tuhuma za kulima na kusafirisha bangi mkoani Mara, baada ya kufanyika operesheni maalum iliyohusisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) pamoja na askari Mgambo.

Operesheni hiyo ilifanyika katika Kanda Maalum ya Tarime Rorya kwenye Bonde la Mto Mara kuanzia Oktoba 2 hadi 8, mwaka huu.

Kamishna Jenerali wa DCEA, Aretas Lyimo akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufanyika kwa operesheni hiyo alisema hekari 807 za mashamba ya bangi ziliteketezwa, magunia 507 ya bangi kavu iliyokuwa tayari kusafirishwa pamoja na magunia 50 ya mbegu za bangi yalikamatwa.

Pia alisema vibanda viwili vidogo vilivyokuwa vikitumika kuchakata na kufunga bangi kabla ya kusafirishwa viliteketezwa.

Lyimo alisema wakazi wa eneo hilo wamelifanya Bonde la Mto Mara kama eneo maalum kwa ajili ya kilimo cha bangi na kujimilikisha kwa kutoruhusu mtu yeyote asiye mkazi kuingia kwenye bonde hilo kama sehemu ya kuficha uhalifu wao.

"Wakazi hao walikuwa wanatishia kumdhuru mtu yeyote atakayeingia ndani ya bonde hilo bila ridhaa yao. Pia, wamediriki kufunga ofisi ya kijiji wakimtuhumu Mtendaji wa Kijiji cha Nkerege kutounga mkono kilimo cha bangi," alisema.

Alisema uwapo wa daraja katika moja wapo ya vijito vinavyopeleka maji Mto Mara hutumika kama kizuizi cha watu kwenda kwenye Hifadhi ya Bonde la Mto Mara maeneo yanayolimwa bangi.

Lyimo alisema ili mtu avuke daraja hilo anatakiwa kujieleza nia na madhumuni ya kuvuka kuelekea upande wa pili, wahusika wasiporidhika na maelezo hawakuruhusu kuendelea na safari.

Aliongeza kuwa hata baadhi ya viongozi wasio waaminifu wa vijiji vinavyopakana na bonde hilo pamoja na wananchi hukodisha na kuuza mashamba ya kulima bangi ndani ya hifadhi ya bonde hilo.

Alisema DCEA kwa kushirikiana na Mkuu wa Mkoa wa Mara na uongozi wa Wilaya ya Tarime watafanya mikutano ya hadhara na kufikiria mipango ya bonde hilo kulindwa dhidi ya kilimo cha bangi na uhalifu mwingine.

Diwani wa Kata ya Tulwa, Chacha Machugu, alisema viongozi wa serikali za mitaa wanaosaidia kuendelea kwa kilimo cha bangi wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria.

Alisema watashirikiana na Jeshi la Polisi kudhibiti bangi kulimwa Tarime na yeyote atakayekiuka miongozo na sheria za nchi atawajibishwa.

**The United Republic of Tanzania**
**President's Office, State House**

### VACANCY ADVERTISEMENT

Tanzania Social Action Fund (TASAF) is currently implementing Productive Social Safety Net Program which aims at protecting the Vulnerable Poor Households from severest consequences of poverty by implementing interventions that will lead to increased Household incomes and opportunities while increasing consumption.

The Permanent Secretary, President's Office, State House is inviting applications from suitably qualified candidates to fill the vacant post of **TASAF Executive Director.**

Job Description and required qualifications for the post is available in TASAF website:- www.tasaf.go.tz

How to apply;

1) a) Applications, enclosing scanned certified copies of certificates and Curriculum Vitae be sent to the following address:-

Permanent Secretary, President's Office
Tanzania Social Action Fund (TASAF)
Kambarage Tower Building
Jakaya Mrisho Kikwete Road
P.O. Box 2719
**DODOMA.**

b) Applications (In PDF Format), enclosing scanned certified copies of certificates, birth certificate and Curriculum Vitae be sent through the following email address: hr@tasaf.go.tz

2) Applications made in a way other than the above will not be considered, Deadline for receiving applications is 10th November, 2023.

PERMANENT SECRETARY
**PRESIDENT'S OFFICE, STATE HOUSE**

217637802

# Mradi wa 2D upatikanaji mafuta hatua za mwisho

**Na Elizabeth Zaya**

MRADI wa kuchukua takwimu za mitetemo zinazojulikana kitaalamu kama 2D katika kitalu cha kutafuta mafuta cha bonde la Eyasi Wembere mkoani Singida, umefikia mwisho huku wataalamu wakieleza kuwa na matumaini ya kuwapo kwa viashiria vya rasilimali ya mafuta katika eneo hilo.

Watafiti wa mafuta katika eneo hilo, walibainisha hayo mwishoni mwa wiki walipotembelewa na maofisa wa Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA).

Mjiofizikia wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) ambaye ni Meneja wa Mradi huo, Sindi Maduhu, alisema utafiti huo umefanyika katika maeneo yaliyoko katika wilaya sita zilizo ndani ya mikoa ya Singida, Arusha, Tabora, Shinyanga na Simiyu.

"Utafiti wa data (takwimu) za mitetemo (2D) ni ule wa kutuma mawimbi ya sauti ardhini na mawimbi hayo hurudisha taarifa ambazo baadaye huchakatwa na kutafsiriwa ili kuielewa miamba ya eneo husika, hivyo kujiridhisha na viashiria vya uwapo wa mafuta.

"Tuna matumaini makubwa kuwa utafiti huu utatusaidia kubainisha na kuainisha maeneo yenye viashiria vya uwapo wa mafuta na gesi asilia na endapo tutagundua viashiria na kujiridhisha na uwapo wa rasilimali hiyo, itaanza hatua muhimu ya kuchoronga visima kwa utafiti zaidi," alisema Maduhu.

Maduhu alisema utafiti wa mafuta kwenye bonde hilo ulianza mwaka 2015 kwa kuchukua taarifa za kijiofizia zilizolenga kusaidia kubaini ukubwa wa eneo la bonde na kuangalia kina cha miamba tabaka iliyopo katika eneo husika.

Alisema eneo hilo la Eyasi Wembere lina kilometa za mraba 10,630 na utafiti huo ulilenga kusoma aina na kina cha miamba ili kubaini uwezekano wa uwapo wa mafuta au gesi asilia katika eneo hilo.

Utafiti katika bonde hilo, alisema umekuwa ukiendelea kufanyika kwa vipindi tofauti na kwa kutumia teknolojia mbalimbali ambapo hadi Julai mwaka huu utafiti wa data za mitetemo kwa njia ya 2D ulianza rasmi katika eneo hilo.

Kuhusu ushiriki wa wazawa kwenye mradi huo, Maduhu alisema wengi wamenufaika na nafasi za ajira katika kipindi chote cha utekelezaji na kwamba mwaka jana zaidi ya Watanzania 40 waliajiriwa kwa ajira za muda ili kufanya kazi ya kukusanya taarifa za kijiokemia.

Alisema kuwa tangu kuanza utafiti huo wa 2D Julai mwaka huu, zaidi ya Watanzania 250 wamepata ajira katika mradi huo huku takriban asilimia 98 ya kazi za kitaalamu zikifanywa na wazawa ikiwa ni pamoja na kazi za kuendesha mitambo huku kazi zinazohusisha raia wa kigeni ikiwa ni asilimia mbili pekee.

"Na katika eneo la ununuzi, zaidi ya asilimia 60 ya kandarasi zilizotumika katika utekelezaji wa mradi huo ni za kampuni za Kitanzania ikiwa ni pamoja na kampuni ya Africa Geophysical Services (AGS) ambayo ndiye mkandarasi aliyefanya utafiti husika wa 2D kwenye mradi huu.

Na kandarasi ndogondogo za kutoa huduma kama chakula, ulinzi na nyinginezo ndizo zilizopewa kipaumbele zaidi kwenye mradi huo ikilinganishwa na kampuni za kigeni," alisema.

Alisema mradi huo katika bonde la Eyasi Wembere, umegharimu Sh. bilioni nane ambazo zimetolewa na serikali kupitia TPDC.

# Taasisi ya Mwalimu Nyerere kushughulikia maadili

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

TAASISI ya Kumbukumbu ya Mwalimu Julius Nyerere, imepanga kupambana na vitendo vya ukatili vinavyotokana na mmomonyoko wa maadili kwa kuzifikia kaya milioni 14 nchini kutoa elimu ya uzalendo na maadili.

Elimu hiyo kwa walengwa, itasaidia jamii kudhibiti mmomonyoko wa maadili ambao kwa kiasi kikubwa unaathiri malezi ya watoto.

Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, Joseph Butiku, akizungumza jana mjini Babati kuelekea wiki ya vijana na kilele cha mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa, alisema tishio hilo limeifanya ije na mradi wake wa kitaifa wa uzalendo na maadili.

Alisema mazungumzo ya viongozi na wananchi yanaonesha kuwa uzalendo na maadili yameporomoka.

"Tumepoteza kwa kiwango kikubwa maadili mwaka jana Septemba, bodi iliambiwa isaidie Watanzania kujadili jambo hili," alisema.

Kwa mujibu wa Butiku, baada ya taasisi hiyo kupewa jukumu hilo na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, aliridhia wajadili uzalendo na maadili kuporomoka.

Alisema katika mradi huo wanataka watu kushiriki kuanzia ngazi ya kaya bila kuangalia mkubwa au mdogo maana wanataka kuelewa maana ya maadili.

"Tunataka bungeni wazungumze wakiwa kama kaya siyo kama wabunge bali wazungumze kama wanakaya," alisema.

Kadhalika, alisema mtu akiwa mzalendo na mwadilifu ni rahisi kuifia kaya yake, taifa na kuzilinda rasilimali za taifa na hatakuwa mla rushwa au kupenda kuwa kiongozi ili ajinufaishe mwenyewe kwa kuwadhulumu wananchi.

Vilevile, alifafanua kuwa uzalendo na maadili vikianzia ngazi ya kaya ni rahisi kudhibiti vitendo viovu katika jamii.

"Tulianza na viongozi wa dini na wote walikiri kuwa maadili na uzalendo umeporomoka na tulipoongea na wazazi nao walikiri kuwa wameshindwa kulea watoto wao," alisema Butiku.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, akisalimiana na Mwakilishi wa Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP), Clara Makenya, kabla ya kuanza kwa kikao baina yake na wawakilishi wa mashirika ya kimataifa yanayofadhili miradi ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi kilichofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# Daladala Kivukoni mwisho Oktoba 20

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), umesema daladala zinazofanya safari kwenye maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam na kumalizia ruti zao Kivukoni, hayataruhusiwa kufika eneo hilo kuanzia Oktoba 20, mwaka huu.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma wa DART, William Gatambi, alisema jana alipozungumza na waandishi wa habari kuwa daladala hizo zimepangiwa vituo vingine vya kuhitimisha safari kupisha upanuzi wa kituo hicho.

Alisema DART inatarajia kuanza ujenzi wa awamu ya nne ya mradi wa mabasi hayo na kuna fungu la kujenga kituo cha Kivukoni kilichojengwa kwenye awamu ya kwanza kinafanyiwa upanuzi ili kumudu kupokea idadi kubwa ya mabasi.

"Mkandarasi anatarajia kuanza ujenzi kwa kuzungusha uzio eneo lile kuanzia Oktoba 15, mwaka huu na ataendelea na maandalizi hadi Oktoba 19. Kwa hiyo daladala zote zilizokuwa zinaishia kituo cha Kivukoni, kuanzia Oktoba 20, mwezi huu, tumezitafutia maeneo mengine ili kupisha upanuzi wa kituo hicho," alisema.

Alitaja vituo vipya ambavyo vitatumiwa na daladala zilizokuwa zinafika Kivukoni kuwa ni maeneo ya ofisi za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Kituo cha zamani cha NBC na Mtaa wa Ohio, jirani na PPF Tower.

Gatambi alisema DART itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu kufungwa kwa kituo hicho kwa siku zilizobaki na aliwataka wenye daladala kuzingatia maelekezo yaliyotolewa na viongozi wa vyama vyao ili kuepusha usumbufu kwa abiria.

Alisema awamu nne za ujenzi wa mradi wa DART zitasababisha mabasi mengi kufika kwenye eneo hilo la Kivukoni, hivyo wameona kuna ulazima wa kukifanyia upanuzi kumudu wingi wa abiria na mabasi yatakayofika hapo.

Gatambi alisema kumekuwa na malalamiko ya abiria kuwa wengi kwenye vituo vya mabasi yaendayo haraka na kwamba hiyo inatokana na ongezeko la watumiaji wa usafiri huo wakati mabasi bado ni yale yale.

"Hata ukiangalia hili ongezeko la mafuta limesababisha watu wengi waache magari yao watumie usafiri wa mwendokasi kwa hiyo serikali inajua kuhusu ongezeko hilo na iko kwenye mchakato wa kuongeza mengine, kuongeza mabasi haya si kama kununua daladala kuna mchakato mrefu," alisema.

Kaimu Katibu Mkuu wa Chama cha Wenye Daladala Dar es Salaam (DARCOBOA), Shifwaa Lema, alisema wanaunga mkono uamuzi huo wa serikali kwani mabadiliko hayo ni ya maendeleo na yenye manufaa kwa umma.

Alisema wanachama wa DARCOBOA walishirikishwa tangu hatua za awali za mchakato wa upanuzi wa kituo hicho na kwa kuwa wameshaonyeshwa maeneo ya kushusha abiria wao watapeana taarifa ili kuepusha usumbufu kwa abiria wanaotumia usafiri huo.

"Maeneo mapya ya kushusha abiria tulishirikishwa wote na tukaridhia, labda tuombe radhi kwa kuwa kutakuwa na usumbufu kidogo tu kwasababu abiria wengine walishazoea kufika Kivukoni na mizigo yao ila wavumilie tu kwani kinachofanyika ni kwa manufaa yetu wote," alisema Lema.

# TANGAZO

**Osho Chemical Industries Ltd.**
**P.O. BOX 16189**
**Near Sunflag Industries Ltd,Opposite police station,Factory Road**
**THEMI, NJIRO**
**ARUSHA , TANZANIA**
**TEL - + 255 757 466 746 + 255 758 888 781**
**EMAIL - tz@oshochem.com**

**AUGUST-2023**
**PRICE LIST FOR**

Pop Vriend Vegetable Seeds PV

osho ®

| ARTICLE | VARIETY | 10 GR SACHETS | 25 GR SACHETS | 50 GR TINS | 100 GR TINS | 250 GR TINS | 500 GR TINS | 1KG TINS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| BEETROOT | DETROIT | 1,000 | 1,500 | | | | | |
| BROCCOLI | CALABRESE | | 4,000 | | | | | |
| CARROT | NANTES 2 | 1,500 | 3,500 | | 12,700 | 24,600 | | |
| CABBAGE | GLORY | | | | | | | |
| CABBAGE | COPENHAGEN | | | | | | | |
| CAULIFLOWER | MERU GIANT | 2,500 | 6,600 | | | | | |
| CELERY | AURORA | 1,500 | 2,600 | 7,000 | | | | |
| CHINESE CABBAGE | MICHIHILI | 1,100 | 1,600 | | | | | |
| CUCUMBER | ASHLEY "C" | | | | | | | |
| EGG PLANT | BLACK BEAUTY | 2,500 | 4,750 | 8,700 | | | | |
| EGG PLANT | LONG PURPLE | 2,500 | 4,750 | | | | | |
| KALE (Sukumawiki) | THOUSAND HEADED | | | | | | | |
| LEEK | ITALIAN GIANT | 2500 | 5,000 | | 18,700 | | | |
| LETTUCE | GREAT LAKES | 2500 | 3,800 | | | | | |
| OKRA (Bamia) | CLEMSON SPINELESS | | 1,600 | | 7,800 | | 0 | 32,600 |
| ONION | RED CREOLE | | 4,200 | | | | | |
| ONION | RED BOMBAY | | | | | | | |
| ONION | TEXAS GRANO 502 | | | | | | | |
| PARSLEY | COMMON | 2,000 | 4,000 | | | | | |
| SWEET PEPPER | YOLO WONDER | 4,000 | 8,000 | 15,600 | 31,000 | | | |
| HOT PEPPER | LONG RED CAYENNE | | | | | | | |
| HOT PEPPER | CARIBEAN RED HABANERO | 16,000 | 21,000 | | | | | |
| HOT PEPPER | CARIBEAN YELLOW HABANERO | 13,500 | | | | | | |
| RADISH | COMET | 1,000 | 1,500 | | | | | |
| SQUASH | GREEN ZUCCHINI | | 4,500 | 8,300 | | | | |
| SQUASH | WALTHAM BUTTERNUT | 2,500 | 4,500 | 8,000 | 15,600 | | | |
| SWISS CHARD | FORDHOOK | 1,500 | 2,500 | | | | | |
| TOMATO | CAL J | | 8,700 | 16,500 | 33,700 | | | |
| TOMATO | RIO GRANDE | 4,500 | 8,500 | 16,800 | 33,400 | | | |
| TURNIP | PURPLE TOP | 1,500 | 2,000 | 4,000 | 8,700 | | | |
| WATER MELON | CRIMSON SWEET | | | | | | | |
| WATER MELON | SUGAR BABY | 1,600 | 2,500 | 5,500 | 10,500 | 22,000 | 41,000 | |
| | | | | | | | | |
| TOMATO MAMBA F1 | MAMBA F1 | | 250 Seeds | 500 seeds | 1000 seeds | | 1000 GRAMS | |
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |
| WATERMELON | KIBOKO F1 | 25grm | 50 Grm | 100 Grm | 250 Grm | 500 Grm | | |
| | | 12500 | 17,300 | 33,000 | 80,200 | 158,000 | | |

**Osho Chemical Industries Ltd.**
**P.O. BOX 16189**
**Near Sunflag Industries Ltd,Opposite police station,Factory Road**
**THEMI, NJIRO**
**ARUSHA , TANZANIA**
**TEL - + 255 757 466 746 + 255 758 888 781**
**EMAIL - tz@oshochem.com**

**PRICE LIST FOR JANUARY 2023**

royalseed

osho ®

| CROP | VARIETY | 10 GR SACHETS | 25 GR SACHETS | 50 GR TINS | 100 GR TINS | 250 GR TINS | 500 GR PACKETS | 1KG PACKETS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Cabbage | Michihili | 1,050.00 | 1,600.00 | 2,600.00 | 4,500.00 | 9,500.00 | 18,000.00 | 32,000.00 |
| Cabbage | Glory of Enkhuizen | 1,300.00 | 2,300.00 | 4,700.00 | 7,600.00 | | | |
| Cabbage | Copenhagen | 1,500.00 | 2,100.00 | 4,000.00 | 7,500.00 | | | |
| Kale | Sukuma Siku | 1,300.00 | 1,800.00 | 4,200.00 | | | | |
| Kale | 1000 Headed | 1,500.00 | 2,700.00 | 4,200.00 | | | | |
| Collards | Southern Georgia | 1,400.00 | 1,900.00 | 3,600.00 | 6,200.00 | | | |
| Spinach | Swisschard Fordhook | 1,300.00 | 1,700.00 | 3,100.00 | 5,500.00 | | | |
| Cucumber | Ashley | 1,900.00 | 3,300.00 | 6,100.00 | 11,700.00 | | | |
| Coriander | Dhania | 1,000.00 | 1,550.00 | 2,900.00 | 5,000.00 | 9,000.00 | 18,800.00 | |
| Lettuce | Maruli | 5,300.00 | 10,200.00 | | 19,900.00 | | | |
| Carrot | Nantes | 1,200.00 | 2,000.00 | 5,750.00 | 10,000.00 | 18,000.00 | 33,500.00 | |
| Okra | Clemson Spineless | 1,100.00 | 1,900.00 | 3,100.00 | 5,500.00 | 10,500.00 | 17,500.00 | |
| Eggplant | Black Beauty | 1,700.00 | 3,600.00 | 6,900.00 | | | | |
| Eggplant | Long Purple | 1,900.00 | 3,900.00 | 7,500.00 | | | | |
| Leeks | Italian Giant | 2,100.00 | 3,800.00 | 7,700.00 | 14,500.00 | | | |
| Squash | Green Zuchini | 1,750.00 | 3,000.00 | 5,250.00 | 9,700.00 | | | |
| Squash | Walthum Butternuts | 2,000.00 | 3,400.00 | 6,200.00 | 10,200.00 | 28,350.00 | | |
| Onion | Red Bombay | 1,600.00 | 2,900.00 | 5,100.00 | 8,500.00 | 18,000.00 | 34,000.00 | |
| Onion | Red Creole | 1,980.00 | 4,000.00 | 7,350.00 | 11,900.00 | 29,000.00 | 56,500.00 | |
| Onion | Texas Grano | | 3,500.00 | | 11,700.00 | | | |
| Tomato | Cal-J | 2,850.00 | 5,200.00 | 11,200.00 | 22,200.00 | | | |
| Tomato | Rio Grand | 3,000.00 | 6,500.00 | 13,000.00 | 25,500.00 | | | |
| Water Melon | Crimson Sweet | 1,900.00 | 3,700.00 | 7,200.00 | 12,200.00 | 28,200.00 | | |
| Water Melon | Sugar Baby | 1,400.00 | 2,800.00 | 4,800.00 | 9,000.00 | 16,300.00 | 29,000.00 | |
| Sweet Pepper | California Wonder | 2,900.00 | 5,200.00 | 10,500.00 | 19,000.00 | | | |
| Sweet Pepper | Maxibell | 700.00 | 16,000.00 | 31,000.00 | 60,200.00 | | | |

**HYBRID SEEDS**

| CROP | VARIETY | 10 GR | 25 GR | 50 GR | 100 GR | 250 GR | 500 GR | 1KG |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Water Melon | Asali F1 | 4,150.00 | 9,000.00 | 27,500.00 | 36,000.00 | 87,000.00 | 174,000.00 | |

| CROP | VARIETY | 2.5 GR | 5 GR | 10 GR | 25 GR | 50 GR | 100 GR | 250GR |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Tomato | Terminator F1 | 28,500.00 | 57,000.00 | 114,500.00 | 280,000.00 | | | |
| Tomato | Rambo | 23,500.00 | 45,000.00 | 90,000.00 | 214,500.00 | | | |
| Tomato | Sandokan F1 | 26,000.00 | 50,000.00 | 97,500.00 | | | | |
| Tomato | Onyx F1 | 10,750.00 | 18,200.00 | 33,250.00 | 81,050.00 | | | |
| Cabbage | Pretoria F1 | | | 16,500.00 | 44,500.00 | 87,000.00 | | |
| sweet pepper | Buffalo f1 | 29,000.00 | 39,000.00 | 71,000.00 | 192,000.00 | | | |

**PROFFESIONAL SEEDS**

| CROP | VARIETY | 100SEEDS | 500SEEDS | 5000 SEEDS | 1000 SEEDS | 5000SEEDS TIN | 100000 SEEDS | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Tomato | Bravo F1 | 20,200 | 90,000 | | 160,000 | | | |
| Onion | Red Coach | | | | | | 190,000.00 | |
| Tomato | Randah | | | | 45,000 | | | |
| Lettuce | CAIPIRIA | | | | | 157,500 | | |

**All Prices are Ex-Arusha Warehouse .**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TRA iendeleze ukaguzi kuepuka bidhaa feki

**HIVI** karibuni Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ilifanya ukaguzi katika baadhi ya kampuni zinazozalisha bidhaa mbalimbali nchini kuangalia kama zinatimiza matakwa ya mamlaka hiyo ya kulipa ushuru na kuiingizia mapato serikali.

Katika ukaguzi huo ilibaini kuwapo kwa stempu za ushuru za kughushi ambazo zinabandikwa kwenye bidhaa kwa lengo la kukwepa ushuru sahihi uliowekwa.

Kibaya zaidi mamlaka hiyo ilibaini kuwa stempu hizo sio zilizotolewa na TRA.

Ukaguzi huo unadhihirisha kuwa kuna haja kwa mamlaka hiyo kufanya ukuguzi wa mara kwa mara kwenye viwanda au kampuni za uzalishaji kubaini kama kuna udanganyifu wowote unaofanyika.

Tunasema hilo kwa sababu katika baadhi ya kampuni zilizofanyiwa ukaguzi kulibainika kuwapo kwa bidhaa nyingi ambazo zilibandikwa stempu ambazo hazikutolewa na TRA.

Hiyo inaonesha kuwa wananchi wanalishwa bidhaa ambazo zinatengenezwa vichochoroni na zisizo na viwango na kubandikwa stempu feki kuonesha kwamba zimekaguliwa na kupitishwa na zinalipa ushuru unaoingia serikalini.

Hata hivyo, imegundulika kuwapo kwa baadhi ya kampuni kukwepa ushuru kwa kutengeneza stempu feki na matokeo yake wanakwepa kulipa ushuru huku serikali ikishindwa kutekeleza baadhi ya miradi ya wananchi muhimu kwa kushindwa kupata fedha za kodi.

Wakati Meneja wa TRA Mkoa wa Arusha, Eva Raphael, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu timu ya mamlaka yake kufanya ukaguzi katika kampuni moja mkoani mwake na kubaini stempu ambazo hazijatolewa na TRA, alisema walifanya ukaguzi wa kawaida wa kuwatembelea wazalishaji bidhaa hizo katika kampuni moja na kukuta katoni zaidi ya 600 zimebandikwa stempu za ushuru na lora moja la stempu zinazodhaniwa za kughushi kutoka katika kampuni hiyo.

Kampuni iliyobainika kufanya ujanja huo ni inayojihusisha na uzalishaji pombe kali, ambapo TRA ilibaini kuwapo zaidi ya katoni 900 zilizozalishwa muda mrefu, lakini hazikubandikwa stempu.

"Timu hii maalum imefanya ukaguzi wa kawaida katika kampuni hii na tumebaini kuwapo stempu hizo za ushuru zinazodhaniwa za kughushi na lora moja, ni hatari sana kwa afya za watumiaji wa bidhaa hizo," alisema.

Kama alivyosema kiongozi huyo wa TRA ni hatari kutengeneza bidhaa kienyeji na kuwalisha wananchi kwa sababu zinakwenda kuathiri afya zao.

Licha ya kuathiri afya, lakini gharama kubwa ya matibabu ili kurudisha ya afya za waliathirika zinarudisha nyuma maendeleo yao na hata serikali inaingia gharama ya kuagiza dawa kutoka nje kuwatibu wananchi wake kwa sababu ya watu wachache wanaopenda utajiri wa haraka haraka.


Wito kwa mamlaka hiyo ni kuwataka wazalishaji wengine kuacha kughushi kwa kuwa ni hatari kwa afya za watumiaji wa bidhaa zao, pia kunasababisha upotevu mapato ya serikali, jambo ambalo ni uhujumu uchumi.

Rais Samia Suluhu Hassan kila mara anapambana ili wananchi anao waongoza wawe na maisha mazuri, wapate huduma bora za kijamii, vyote vinatokana na kodi zinazotolewa na wananchi. Suala la uzalendo lazima liwapo katika ulipaji kodi.

Vilevile, wazalishaji wanatakiwa kuwa wazalendo kwa kufuata sheria zinazowaongoza kutekeleza majukumu yao ya uzalishaji bidhaa zao ili kuepuka usumbufu.

Wananchi pia wanatakiwa kuhakiki bidhaa za vinywaji kwa kutumia Hakiki App kabla ya kutumia bidhaa hizo kwa manufaa yao. Na vile vile wanapobaini udanganyifu wa aina yoyote, hawana budi kutoa taarifa kwa sababu athari zinawapata Watanzania wote.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Neema Msalaba

## Muungwana Lazima Nilonge

# Dawa za kulevya iwe vita endelevu

**DAWA** za kulevya na ulevi wa kupindukia ni tatizo kubwa linalowakumba vijana wengi katika jamii nyingi duniani na hata Tanzania pia.

Matumizi ya dawa hizo na pombe yanaelezwa kuwa na madhara makubwa ya kiafya, kijamii na kiuchumi na si jambo la kupuuzwa.

Elimu ndiyo silaha kuu dhidi ya dawa za kulevya na vijana wanapaswa kufahamishwa kuhusu athari za dawa na ulevi wa kupindukia ambao sasa unasambaa karibu nchi nzima shuleni, vyuoni na ndani ya jamii zinatakiwa kuanza sasa kwa kuwa mstari wa mbele katika kutoa na kuhamasisha vijana kuachana na matumizi ya vitu hivyo hatarishi kwa kutoa elimu endelevu ya matokeo hasi ya kemikali hizo.

Familia, shule na jamii ndizo msaada mkubwa katika kutoa mwelekeo bora kwa vijana, wazazi na walezi ambao ndiyo familia imara wanaweza kuwa kizuizi kikubwa dhidi ya vishawishi vya tabia zinazosababisha vijana kupotea.

Kwa ujumla vijana wanatumbukia katika janga hili wanapaswa kupewa nasaha, kukemewa na kupatiwa mwelekeo sahihi wa kuachana na jambo hili ili waepuke madhara yanayojitokeza au yatakayojitokeza.

Vijana wanapopata fursa za kujihusisha na shughuli mbalimbali kama vile michezo, sanaa na miradi ya kijamii, wanakuwa na mwelekeo bora zaidi katika maisha yao na hivyo kupunguza vishawishi vya dawa ya kulevya kuanzia bangi, mihadarati na ulevi wa pombe kali kila wakati.

Hivyo serikali kwa kushirikiana na wadau wengine wanapaswa kuanzisha miradi ya kiuchumi kuliko kuwahimiza wajiajiri ili hali wengine hawana mitaji hali inayowatumbukiza kwenye janga hilo kutokana na msongo wa mawazo na maisha magumu, lakini na umaskini unaowafanya kushindwa kumudu maisha yao.

Baadhi ya vijana wanajikuta wakitegemea dawa hizo na ulevi kutokana na changamoto za afya ya akili. Kuimarisha huduma za afya ya akili kunaweza kusaidia kutambua na kutibu matatizo haya mapema. Pia kijana mwenye awe binti au mwanaume anapaswa kuwa muwazi iwapo atapata tatizo kwa kuwaeleza watu wake wa karibu na anaowaamini ili kusaidika mapema na kuepuka kuingia katika janga hilo.

Kuwapo kwa vituo vingi vya tiba na msaada kwa wanaotumia dawa ya kulevya kunaweza kuwasaidia wengi kujinasua kutoka kwenye janga hili. Vilevile serikali ijenge vituo vingi na iwaunge mkono watu na mashirika binafsi yanayowasaidia vijana walioathirika na tatizo hilo kwa kutenga bajeti zinazotosheleza.

Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa sheria zinazohusiana na kuzalisha, kuuza na kutumia dawa ya kulevya zinatekelezwa kikamilifu. Mahakama nazo zitoe adhabu kali kwa wote watakaothibitika na kujishirikisha na dawa na ulevi wa kupindukia ili kudhibiti tabia hiyo ambayo sasa inakoo kila mahali.

Vijana wenyewe wanaweza kuwa sehemu ya suluhisho, kupitia vikundi vya ushauri, wanaweza kushirikiana pamoja kupambana na dawa za kulevya, aidha utafiti zaidi unahitajika ili kuelewa kwa kina sababu zinazochangia matumizi yake miongoni mwa vijana na hivyo kutafuta suluhisho endelevu na kuimarisha vyombo vya kukabiliana na hali hiyo.

Programu za kinga zinazolenga kutoa mafunzo kwa vijana kuhusu hatari za tabia hizo za kutumia vilevi kupindukia zinaweza kusaidia kuzuia matumizi ya dawa hizo zikitolewa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Ikumbukwe kuwa dawa za kulevya mara nyingi huvuka mipaka ya mataifa hivyo ushirikiano wa kimataifa unaweza kuwa na manufaa makubwa katika kupambana na biashara na utumiaji wa vitu hivyo ambavyo vinaathiri vijana na kuteketeza nguvu kazi.

Kuepuka matumizi yake na ulevi wa kupindukia si kazi ya mtu mmoja au taasisi pekee bali ni ushirikiano wa juhudi za pamoja kutoka kwa jamii nzima, ikiwamo familia, shule, taasisi za kijamii, serikali, na vijana wenyewe, asasi za kidini, vyombo vya usalama, kwa pamoja, wanaweza kufikia kupatikana jamii ambayo vijana watakuwa salama dhidi ya madhara ya dawa na pombe.

## DCEA yateketeza zaidi ya hekari 800 za bangi

**Na Kulwa Mzee**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, Jeshi la Kujenga Taifa, Mgambo pamoja na vyombo vingine vya dola, imeteketeza hekari 807 za mashamba ya bangi na kukamata magunia 507 ya bangi kavu.

Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Aretas Lyimo, alisema operesheni hiyo maalum imefanyika mkoani Mara hususani katika kanda maalum ya Tarime Rorya kwenye Bonde la Mto Mara.

Alisema operesheni hiyo ilifanyika kuanzia Oktoba 2 hadi 8, mwaka huu na walifanikiwa pia kukamata gunia 50 za mbegu za bangi pamoja na kuteketeza viwanda viwili vidogo vilivyokuwa vikitumika kuchakata na kufunga bangi kabla ya kusafirishwa na kwamba watuhumiwa 11 wanashikiliwa kuhusika na dawa hizo.

Alisema, wakazi wa eneo hilo wamelifanya Bonde la Mto Mara kama eneo maalum kwa ajili ya kilimo cha bangi na kujimilikisha kwa kutoruhusu mtu yeyote asiye mkazi kuingia kwenye bonde kama sehemu ya kuficha uhalifu wao na wanawatishia kumdhuru yeyote atakayeingia ndani ya bonde hilo bila ridhaa yao.

"Wamediriki kufunga ofisi ya kijiji wakimtuhumu mtendaji wa kijiji cha Nkerege kutounga mkono kilimo cha bangi. "Kitendo kinachofanywa na wananchi waliopo katika eneo la mto Mara ni kinyume na sheria, viongozi wa serikali na wananchi ambao sio wakazi wa hapa hawaruhusiwi kuingia eneo la bonde," alisema Lyimo.

Alisema kuwapo kwa daraja lililopo katika moja wapo ya vijito vinavyopeleka maji mto Mara, linatumika kama kizuizi cha watu kwenda kwenye hifadhi ya bonde la mto maeneo yanayolimwa bangi. Ili mtu avuke anatakiwa kujieleza nia na madhumuni ya kuvuka kuelekea upande wa pili, na wahusika wasiporidhika na maelezo hawaruhusu kuendelea na safari.

Kamishna Jenerali Lyimo anaomba wizara zinazohusika kushirikiana na Mamlaka kutokomeza kilimo cha bangi katika eneo hilo kwa kuwa mbali na operesheni iliyofanyika bado mashamba ya bangi ni mengi pembezoni mwa mto na wananchi wanatumia maji ya mto kumwagilia.

Pia, Kamishna Lyimo alisema, Mamlaka kwa kushirikiana na Mkuu wa Mkoa wa Mara na uongozi wa Wilaya ya Tarime, watafanya mikutano ya hadhara na kufikiria kuwa na mipango kabambe kuona ni namna gani bonde litalindwa dhidi ya kilimo cha bangi na uhalifu mwingine.

"Sisi kama mamlaka tutafanya operesheni endelevu katika maeneo haya kuhakikisha kilimo cha bangi kinaisha. Bonde hili lina rutuba nyingi na linakubali mazao ya aina zote, hivyo tumekubaliana na Mkuu wa Mkoa wa Mara kuwa na mikakati ya kusimamia bonde ili kumaliza kilimo cha bangi na kutafutwa kwa shughuli nyingine ambayo itakuwa rafiki," alisema Lyimo.

Diwani wa Kata ya Tulwa, Chacha Machugu alisema, viongozi wa serikali za mitaa wanaosaidia kuendelea kwa kilimo cha bangi wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria ili iwe fundisho kwa watu wengine.

Aliwaomba viongozi wa dini kusaidia kuwaambia waumini wao kuwa dawa za kulevya hazitakiwi.

"Tutashirikiana na Jeshi la Polisi kuhakikisha bangi hailimwi Tarime na yeyote atakaye kiuka miongozo na sheria za nchi atawajibishwa kwani sote tunaongozwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," alisema Chacha.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango-Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salum (kulia), ambaye anaongoza ujumbe wa Tanzania katika mikutano ya mwaka ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), kwa niaba ya Waziri wa Fedha wa Tanzania, Dk. Mwigulu Nchemba, akiagana na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Fedha la Kimataifa, (IMF) anayewakilisha Kundi la Kwanza la Nchi za Afrika, Willie Nakunyada, baada ya kufanya mazungumzo mjini Marrakech, nchini Morocco jana. **PICHA: WIZARA YA FEDHA**

# Biteko awataka watendaji serikalini kufanya kazi bila kusukumwa

**Na Joseph Mwendapole**

NAIBU Waziri Mkuu, Dk. Doto Biteko, amewataka watendaji wa serikali kuwa wabunifu na kutekeleza mipango wanayoweka kwa wakati badala ya kusubiri kusukumwa.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza kwenye Jukwaa la Uwekezaji Pangani, lililofanyika pembeni mwa maonyesho ya Kimataifa ya Swahili International Tourism Expo (SITE).

Jukwaa hilo liliandaliwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kwa kushirikiana na Ofisi ya Wilaya ya Pangani Mkoa wa Tanga.

Biteko alisema watendaji wanapaswa kwenda chini kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua kwa haraka badala ya kusubiri kero ndogo kufikishwa kwa Rais na viongozi wengine wa ngazi za juu.

"Tumwache Rais afikiri kuhusu mambo makubwa makubwa tu kama ujenzi wa reli ya kisasa na mengine kwa hiyo haya madogo madogo ambayo yako ndani ya uwezo wetu tuyatatue tusisubiri kushurutishwa na mtu," alisema.

Alisema imekuwa kawaida kuona viongozi wakiweka msukumo mkubwa kwenye mambo makubwa ya kitaifa na kusahau kabisa mambo madogo yanayogusa moja kwa moja maisha ya wananchi wa hali ya chini.

Alisema Wilaya ya Pangani imekuwa ya mfano kwa kuanzisha Jukwaa la Uwekezaji ambalo litakuwa na manufaa makubwa kuvutia utalii na uwekezaji na alizitaka wilaya zingine kote nchini kuiga mfano huo.

Alisema ipo kasumba kwa baadhi ya viongozi kukatisha tamaa viongozi wa ngazi za chini wanapoonyesha ubunifu hali ambayo alisema inachelewesha maendeleo na kukwamisha miradi.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akifanya jitihada mbalimbali kutangaza utalii na kwamba viongozi hawapaswi kumwacha peke yake.

Mkurugenzi wa Idara ya Uhamasishaji Utalii wa TIC, John Mnali, alisema Wilaya ya Pangani ina fursa nyingi za uwekezaji kama kilimo biashara, uchumi wa buluu na utalii kutokana na Mbuga ya Saadani.

Alisema, TIC imekuwa ikitoa vivutio mbalimbali kwa wawekezaji kulingana na aina ya uwekezaji ambao mtu anataka kuwekeza na kwamba wale wanaouza nje bidhaa zao kwa asilimia 80 wamekuwa na vivutio vya peke yao tofauti na wale wanaozalisha na kuuza ndani.

Mkuu wa Wilaya ya Pangani, Zainab Abdalah, aliipongeza TIC kwa namna ambavyo wamefanikisha Jukwaa la Uwekezaji Pangani ambalo ni la kwanza kufanyika kwa ngazi ya wilaya nchini.

Alisema Wilaya ya Pangani imekaa kimkakati na imejaaliwa kuwa na fursa nyingi za uwekezaji huku akiahidi hakuna mwekezaji atakayekwenda kwenye wilaya hiyo kwa nia ya kuwekeza ambaye atakutana na vikwazo.

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Hashim Komba, alisema maonyesho ya siku tatu ya SITE ni ushahidi ambavyo Rais Samia anaendelea kufungua uchumi na fursa mbalimbali.

Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile, alisema serikali inajitahidi kufanya mageuzi makubwa kwenye sekta ya usafirishaji na uchukuzi ili kuvutia uwekezaji na uzalishaji wa bidhaa mbalimbali nchini.

Alisema Tanzania ina bandari 693, lakini zilizorasimishwa ni 86 pekee na serikali inaendelea na jitihada za kurasimisha bandari zote ili zisaidie kuliingizia taifa kipato.


Naibu Waziri wa Utalii, Danstan Kitandula, alisema kuna jitihada kubwa zinafanywa na serikali kuongeza mchango wa sekta ya utalii kwenye pato la taifa kutoka asilimia 16 ya sasa.

Mkurugenzi wa Bodi ya Utalii (TTB), Damas Mfugale, alisema Wilaya ya Pangani imekaa kimkakati na bodi inajipanga kuandaa master plan itakayotumika kuendeleza utalii wake.

Alisema bodi yake pia itawekeza kwenye kuendeleza utalii wa fukwe kwani Tanzania imejaaliwa kuwa na fukwe yenye urefu wa kilomita 1,440 ambayo ikitumika vizuri italiingizia taifa kipato.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Serikali kushirikiana na wadau kukabiliana tatizo afya ya akili

**Na Frank Monyo**

SERIKALI imejipanga kushirikiana na wadau mbalimbali kukabiliana na tatizo la afya ya akili kwa Watanzania wengi hususan kwenye maeneo ya kazi.

Mpango huo umeelezwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu-Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, alipokuwa akiwahutubia wanamichezo walioshiriki Bonanza la Waajiri lililoandaliwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), jijini Dar es Salaam.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na wadau kuweka mipango ya kisera na kuimarisha miundombinu ya utoaji huduma kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kujenga vituo vya afya nchi nzima na kuongeza wataalam wa afya ya akili kwenye vituo hivyo.

"Ninafahamu licha ya uwapo wa changamoto ya afya ya akili, wafanyakazi katika maeneo yao ya kazi wamekuwa wakikabiliwa na tishio la magonjwa yasiyoambukiza kama vile, saratani, magonjwa ya moyo na kisukari.

Magonjwa haya kwa kiasi kikubwa yanasababishwa na mtindo wa maisha tunayoishi na kutokuwa na tabia ya kufanya mazoezi ya viungo vya miili yetu," alisema Waziri Ndalichako.

Alishauri wananchi kufuata mitindo mizuri ya afya ikiwamo kula milo kamili na kufuata ushauri wa wataalamu wa afya. "Niwahimize waajiri kuendelea kuwekeza katika michezo na programu mbalimbali zinazojenga tabia ya kufanya mazoezi ya viungo."

Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Mhandisi Cyprian Luhemeja, pamoja na kuwapongeza ATE kwa kuandaa Bonanza hilo, alisema:

"Bonanza hili ni changamoto kwetu kama wizara yenye dhamana ya masuala ya ajira na vijana ambapo ndio tulipaswa kuandaa vitu kama hivi hivyo nasi tutakwenda kujipanga na kuona ni kwa namna gani tutaweza kuwa na matukio kama haya kwa lengo la kuwaendeleza vijana katika nchi yetu," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya taasisi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Khadija Mwenda, alisema kutokana na ukubwa wa tatizo la magonjwa yasiyoambukiza miongoni mwa waajiri na wafanyakazi kwasasa ni wakati mwafaka kwa wadau na serikali kushirikiana kushughulikia tatizo hilo.



Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga akizindua umeme uliowashwa kwa mara ya kwanza katika Kata ya Nlitumbandyosi, wilayani Mbinga. **PICHA: GIDEON MWAKANOSYA**

# KEC yatoa mafunzo ya ujuzi kwa vijana 46

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

SHIRIKA la Elimu Kibaha (KEC) kupitia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi (Kibaha-FDC) kwa kushirikiana na Chuo cha Biashara Kibaha (Kibaha Institute of Business-KiB) kimeanza kutoa mafunzo ya ujuzi kupitia kozi za muda mfupi kwa vijana wenye umri wa miaka 15-19.

Mafunzo hayo yanatolewa chini ya Mradi wa AHADI unaofadhiliwa na Serikali ya Canada (Global Affairs Canada) na kusimamiwa na World Vision. Unatekelezwa na taasisi mbalimbali ambazo ni Kibaha Institute of Business, Babawatoto, KIWOHEDE and Medicines du Monde (MdM).

Katika mradi huo, KiB inawawezesha vijana balehe katika masuala ya kiuchumi kupitia mafunzo ya ujasiriamali, ushauri wa kibiashara, kuwaunganisha vijana na fursa za mitaji ya biashara na ajira na kuimarisha ushiriki wa vijana katika mijadala ya kisera.

Mafunzo hayo ya muda mfupi yanayoendeshwa na Kibaha- FDC na KiB, yalifunguliwa rasmi na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Elimu Kibaha (KEC), Anathe Nnko na kuhusisha vijana 46 kwa awamu ya kwanza, huku asilimia zaidi ya 60 wakiwa ni wasichana.

Akifungua mafunzo hayo, Nnko alikishukuru chuo cha KiB na World Vision kwa kuchagua kushirikiana na Shirika la Elimu Kibaha kupitia Kibaha-FDC katika kutoa mafunzo ya muda mfupi katika fani za hotelia, ufundi magari, udereva, useremala, mapambo, ushonaji na ubunifu wa mitindo pamoja na urembo na ususi.

Nnko aliwapongeza vijana balehe wanaonufaika na mradi wa AHADI na kuwaasa kuzingatia mafunzo kwa vitendo ili kujiimarisha kiujuzi na hatimaye waweze kujiajiri na kuajiri watu wengine baada ya kumaliza mafunzo hayo. Vilevile, aliwahimiza vijana hao kuwa na nidhamu wakati wa mafunzo.

Mratibu wa Mradi wa AHADI kutoka World Vision, Eveline Sanga, aliwataka wanufaika hao wa AHADI kuwa makini darasani ili mafunzo watakayoyapata yawasaidie kupata kipato ambacho hatimaye kitaboresha maisha yao jambo ambalo ndiyo lengo kuu la mradi.

Mwenyekiti wa Bodi wa Chuo cha KiB, Prof. Lemayon Melyoki, alikishukuru Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha (Kibaha-FDC) kwa kukubali kushirikiana na Chuo cha KiB kutoa mafunzo ya ujuzi kwa vitendo chini ya Mradi wa AHADI.

Alisema mafunzo hayo yatachangia kwa kiwango kikubwa kufikia malengo ya mradi hasa katika kujenga uwezo wa kiuchumi kwa vijana. Pia, aliwaasa wanufaika kujituma vizuri wakati wa mafunzo ili waweze kupata ujuzi walioknwenda kujifunza Kibaha-FDC.

Mnufaika wa mradi wa AHADI, Rosemary Emily aliahidi kutoa ushirikiano kwa walimu na wanafunzi wa Kibaha- FDC wakati mafunzo hayo.

## Kijiji chapata umeme kwa mara ya kwanza tangu Uhuru

**Na Gideon Mwakanosya,** MBINGA

NAIBU Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, amezindua na kuwasha umeme katika Kijiji cha Litumbandyosi, Kata ya Litumbandyosi Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Vijijini mkoani Ruvuma, huduma ambayo haijawahi kupatikana tangu Uhuru.

Umeme huo ambao umewashwa juzi na kushuhudiwa na wananchi kutoka katika vijiji vinne vya kata hiyo ambavyo ni Kingole, Mabuni, Luhagara na Litumbandyosi umetokana na mtambo wa kuzalishia umeme toka Wakala wa Umeme Vijijini (REA).

Akizungumza na wananchi kwenye uzinduzi huo, Naibu waziri alisema kuwa umeme huo kwa awamu ya kwanza utawashwa kilometa moja na awamu ya pili utawashwa kilometa mbili na tayari serikali imeshatoa fedha kwa miradi yote miwili.

Alisema kuwa huduma za nishati za umeme vijijini (REA)ni muhimu kwa sababu wananchi wamekuwa wakijishughulisha na shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kuanzisha viwanda vidogo vidogo kwa lengo la kujiletea maendeleo.

Kapinga alisema umeme huo utazalisha nishati itakayokidhi mahitaji ya wananchi wa vijiji vya kata hiyo na vitongoji vyake na kuwafanya waondokane na adha ya kukosa huduma hiyo kwa miaka mingi.

"Ndugu zangu wa vijiji vilivyobakia niwahakikishie nyote mtapata umeme kwa sababu Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, amekwisha toa fedha kwa vijiji vyote vilivyobakia hakupepesa macho alisema anataka kumaliza vijiji vyote changamoto ya umeme na fedha imeshatoka," alisema Kapinga.

Hata hivyo, amesikitishwa na kasi ndogo ya mkandarasi Namis Corporate Limited Shaidu Rutakolezibwa, kutokana na kuchelewesha kukamilishwa kwa miradi hiyo ya REA kwa wakati jambo ambalo linachelewesha maendeleo kwa wananchi ambao wengi wao ni maskini.

Alisema mkandarasi akimaliza kazi zake analipwa na kuhoji kwanini umeme usiende kwa kadiri alivyotakiwa kupeleka.

Kadhalika, alisema hatakubaliana na uzembe wa aina yoyote na kuagiza hadi kufikia Oktoba 30 vijiji vyote vya awamu ya kwanza viwe vimeshawashwa umeme.

Wanakijiji hao wameishukuru serikali kwa kuwaletea mradi wa huo ambao utaleta tija kubwa kwa wananchi ambao wapo mbali na mjini na utawawezesha kuchakata bidhaa zao hapo hapo kijijini badala ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za umeme.

Aliomba serikali kuharakisha kusambaza umeme huo kwa wananchi na taasisi za serikali ikiwamo zahanati, kituo cha afya, shule na ofisi za chama na serikali ili uweze kuleta tija.



# Wadau zaidi 700 Afrika kukutana Arusha kujadili haki za binadamu

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WADAU zaidi ya 700 kutoka mataifa mbalimbali Afrika, wanatarajiwa kushiriki katika kikao cha 77 cha Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kuanzia Oktoba 20 hadi Novemba 9 mwaka huu jijini hapa.

Kikao hicho cha siku 20 kitafanyika katika Kituo cha Kimataifa wa Mikutano Arusha (AICC) na kitafunguliwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Waziri wa Katiba na Sheria, Balozi Dk.Pindi Chana, alitoa taarifa hiyo ya awali jana Jijini hapa, kuhusu maandalizi ya mkutano huo.

Balozi Chana alisema kikao hicho cha kawaida kitajadili masuala mbalimbali ikiwemo hali ya haki za binadamu Afrika, taarifa za wanaharakati wa haki za binadamu, msaada wa kisheria na upatikanaji wa haki Tanzania.

Pia, kitajadili uzinduzi wa nyaraka mbalimbali za kamisheni hiyo na maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu Afrika kwa kuzingatia Itifaki ya Maputo.

"Kikao hicho kitajadili masuala ya msingi yanayohusu haki za binadamu na watu, tutapata fursa siyo tu ya kubadilishana uzoefu wa masuala ya haki za binadamu na watu, lakini pia kuitangaza nchi kwa mataifa mbalimbali juu ya utajiri na rasilimali tulizonazo," alisema.

Alisema awali Januari 31, mwaka huu, Mwenyekiti wa Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Kamishna Remy Lumbu kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), alimtembelea Rais Samia na kuomba Serikali ya Tanzania iwe mwenyeji wa kikao hicho.

"Wizara ya Katiba na Sheria kama Wizara yenye kuratibu na kusimamia masuala ya haki za binadamu na watu nchini, inaendelea na maandalizi ya kikao hicho ambacho kitahusisha sekta mbalimbali zaidi ya masuala ya haki za binadamu na watu yakiwemo masuala ya ushirikiano wa kimataifa, utamaduni, sanaa na michezo, fedha na uchumi, ulinzi na usalama,afya na habari na mawasiliano,"alisema Waziri Chana.

Alisema Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu inapaswa kutekeleza majukumu makuu matatu ambayo ni ulinzi wa haki za binadamu na watu, kukuza haki za binadamu na watu na kutoa tafsiri ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu.

Akijibu swali kutoka kwa waandishi wa habari kuhusu Tanzania kujitoa katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu pamoja na wananchi wa nchi hiyo na taasisi mbalimbali kutokufungua kesi katika Mahakama hiyo, alisema kuna mazungumzo yanaendelea kufanyika kati ya Serikali na Mahakama.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Khatibu Kazungu, alisema moja ya masuala ambayo serikali inajivunia ni pamoja na kampeni ya msaada wa kisheria inayoitwa Mama Samia Legal Aid, ambayo imeanza kutekelezwa mwaka huu.

Alisema kampeni hiyo imejikita katika kutoa elimu ya kisheria na msaada wa kisheria kwa wananchi katika masuala mbalimbali, inayotekelezwa na wizara hiyo kwa kushirikiana na asasi za kiraia na wadau wengine.

## PBWB yapata dawa ya kudhibiti mafuriko Mto Rau

**Na Mary Mosha,** MOSHI

ADHA ya mafuriko yanayotokana na kufurika maji ya Mto Rau na kusababisha athari kwa wananchi wa Kijiji cha Mandaka Mnono, katika eneo la Moshi Vijijini mkoani Kilimanjaro, limepata mwarobaini.

Mkurugenzi wa Bodi ya Maji Bonde la Pangani (PBWB), Segule Segule, alisema serikali imelazimika kuongeza kina na upana wa mto huo ili kuzuia mafuriko.

Segule alisema hayo jana alipokwenda kukagua kazi ya kuongeza kina cha mto huo, baada ya kuathiriwa na shughuli za kibinadamu kwa muda mrefu.

Alisema, upanuzi wa mto huo unaopeleka maji katika Bwawa la Nyumba ya Mungu ni sehemu ya utekelezaji wa agizo la Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Viongozi hao wakuu walitoa agizo hilo baada ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), kutoa angalizo kwa baadhi ya mikoa nchini kukumbwa na mvua za El-Nino.

Kwa mujibu wa Segule, pia ni jukumu la bodi kulinda vyanzo vya maji na kutaka jumuiya za watumia maji na serikali za vijiji kulinda vyanzo hivyo.

Naye, Mwenyekiti wa Kijiji Cha Mandaka Mnono, Mdekio Temba, aliwataka wananchi kutunza miundombinu ya mto huo kwa kuwa gharama zinazotumika ni kubwa.

Alisema mafuriko yamekuwa yakiathiri kaya 185 katika vitongoji vya Uswahilini na Saningo vyenye jumla ya kaya 338.

Diwani wa Viti Maalumu, Theresia Mlay, alisema waathirika zaidi wa mafuriko hayo ni wanawake wazee na watoto.

**Viongozi hao wakuu walitoa agizo hilo baada ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), kutoa angalizo kwa baadhi ya mikoa nchini kukumbwa na mvua za El-Nino.**



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (katikati), akifurahia jambo na mkimbiza Mwenge wa Uhuru kitaifa, Emmanuel Hondi, wilayani Kiteto juzi, kulia ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Peter Toima. Mwenge huo unatarajiwa kuhitimisha mbio zake kitaifa Mjini Babati Oktoba 14. **PICHA: GIFT THADEY**

# Kituo chajenga madarasa kusaidia watoto wasiojiweza

**Na Allan Isack,** HAI

KITUO cha Maendeleo ya Mtoto na Kijana Elishadai kilichoko Mailisita Wilaya ya Hai, mkoni Kilimanjaro, kimejenga vyumba vitano vya madarasa kwa ajili ya kusaidia watoto wanaotoka katika mazingira magumu wapate elimu na mafunzo ya ufundi.

Kituo hicho kiko chini ya Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG), ujenzi huo umegharimu Sh.milioni 123.

Mradi huo umefadhiliwa na Shirika la Compassion Tanzania kwa kushirikiana na Compassion International Korea, Kanisa Kimataifa la Saeronam la Korea Kusini.

Mratibu wa kituo hicho, Amani Ndelwa, akitoa taarifa ya maendeleo ya mradi huo, kwa raia wa kigeni 22 kutoka Kanisa la Kimataifa la Saeronam, wakiwamo wanafunzi 19, alisema kundi la wanafunzi limechangia zaidi ya Sh.milioni 100.

"Vijana hawa wanaotoka katika familia zinazofadhili watoto, wako hapa nchini kujifunza kazi zinazofanywa na Shirika la Compassion Tanzania kuwafungua watoto na vijana kutoka katika minyororo ya umaskini, pia watakutana watoto waliofadhiliwa pamoja na kuzitembelea familia zao," alisema.


Mwakilishi wa Shirika la Compassion Tanzania, Benson Mushi, alisema hadi sasa watoto 7,466 kutoka familia zinazokabiliwa na umaskini Tanzania wanafadhiliwa na shirika hilo kwa upande wa Korea Kusini, huku watoto 1,550 wakifadhiliwa na Kanisa Kimataifa la Saeronam.

**Kituo hicho kiko chini ya Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG), ujenzi huo umegharimu Sh.milioni 123.**

Mchungaji Kiongozi wa TAG Mailisita Elishadai, Semu Bukuku, alisema awali walikuwa wana uhaba wa vyumba vya madarasa ambapo waligawa wanafunzi makundi mawili.

"Tunawashukuru wenzetu wa Korea kwa msaada huu wa ujenzi wa miundombinu ya madarasa hivyo tunaamini idadi ya watoto tunaowaandikisha itaongezeka,"alisema.

Alisema kundi la kwanza waliosomea kanisani hapo na wengine waliwaombea Shule ya Msingi Njoro.



# Vijana watakiwa kuchangamkia fursa sekta ya kilimo, mifugo

**Na Alex Sayi** MASWA

VIJANA wametakiwa kuchangamkia fursa za ajira zaidi ya 500,000 zilizopo katika sekta ya kilimo na mifugo ili kukabiliana na kero ya uhaba wa ajira nchini.

Hayo yamesemwa na Mwenyekiti wa kikundi cha vijana cha Agriween cha wilayani Maswa mkoani Simiyu, Peter Paschal wakati wa kongamano la vijana lililofanyika katika halmashauri hiyo, likiwa na lengo la kubaini fursa zilizopo za ajira kwa vijana.

Paschal alisema kuwa vijana kati ya 400,000 hadi 600,000 huachwa bila ajira kila mwaka kutokana na uhaba wa ajira uliopo kwa sasa nchini, hivyo kuwataka vijana kuchangamkia fursa za ajira kwenye sekta ya kilimo na ufugaji.

"Takwimu za mwaka 2011 toka Ofisi ya Taifa ya Takwimu inaonesha kuwa vijana wanaoingia kwenye soko la ajira kila mwaka ni 800,000 hadi 1,000,000, wanapigania nafasi za ajira 60,000 katika sekta ya umma na takribani nafasi 300,000 katika sekta binafsi." alisema.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Taifa (CCWT), Kusundwa Wamalwa alisema kuwa chama hicho kwa sasa kinaendelea na makubalianao na taasisi za benki ili wafugaji na wakulima waweze kukopesheka.

Mkuu wa Wilaya ya Maswa, Aswege Kaminyoge alisema kuwa Rais Samia Suluhu Hassan tayari ameshatoa fedha kwa benki zote nchini ili vijana, wakulima na wafugaji waweze kukopesheka.

"Kwa ukanda huu wa Simiyu suala la marisho kwa mifugo ni changamoto, Rais Samia ameshaliona hilo na ametoa fedha kwa ajiri ya kuanzisha mashamba ya majani ya marisho, hivyo vijana changamkieni fursa hii mlime na baadae mje kuwauzia wafugaji" alisema.

**"Takwimu za mwaka 2011 toka Ofisi ya Taifa ya Takwimu inaonesha kuwa vijana wanaoingia kwenye soko la ajira kila mwaka ni 800,000 hadi 1,000,000..."**

Mkuu wa Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Robert Urasa akizungumzia upatikana wa mbegu alisema kuwa halmashauri inajipanga kununua mbegu kwa ajili ya kuwasambazia bure wafugaji watakoa kuwa wanahitaji.

Mkulima na mfugaji wilayani hapa, Philibet Akili aliiomba halmashauri hiyo kupitia ofisi ya kilimo kupunguza urasimu wa upatikanaji wa mbegu za majani ya marisho kwa madai kuwa wamekuwa wakifika kwenye ofisi hizo za kilimo wanakosa taarifa sahihi ya upatikanaji wa mbegu.



Askari wa Jeshi la Kujenga Taifa, Mgambo pamoja maofisa wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) wakiwa katika operesheni ya kuteketeza mashamba ya bangi mkoani Mara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Siku ya Mbolea Duniani kuadhimishwa kitaifa Tabora

**Na Waandishi Wetu**

TANZANIA inatarajiwa kuungana na mataifa mengine ulimwenguni kuadhimisha Siku ya Mbolea Duniani itakayofanyika kitaifa mkoani Tabora kuanzia Oktoba 11 hadi 13 mwaka huu katika Uwanja wa Chipukizi.

Katika maadhimisho hayo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe.

Taarifa ya maadhimisho hayo imetolewa jana kwa vyombo vya habari na Mkuu wa Mkoa huo, Balozi Dk. Batilda Burian na kutaja maadhimisho hayo kuwa muhimu kutokana na fursa mbalimbali za wakulima na sekta nyingine zitakazoibuliwa.

Alibainisha kuwa maadhimisho hayo yataambatana na maonesho ya bidhaa mbalimbali za wakulima ikiwemo pembejeo (mbolea, mbegu na viuatilifu zitakazooneshwa na kampuni zinazouza pembejeo hapa nchini.

Batilda aliongeza kuwa kampuni zaidi ya 15 zinazojihusisha na uagizaji na uuzaji mbolea nchini, mashirika na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Kilimo na taasisi za fedha ni miongoni mwa wadau watakaoshiriki maonesho hayo.

Alisema, kaulimbiu ya maadhimisho hayo ni 'Agenda 10/30: Matumizi sahihi ya mbolea ya ruzuku kwa kilimo chenye tija' kauli ambayo imebeba ujumbe wenye matumaini mapana kwa wakulima.

Aidha, katika taarifa iliyotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea nchini (TFRA) Kanda ya Kati ilieleza kuwa katika maadhimisho hayo wakulima watapata fursa ya kupata elimu ya matumizi sahihi ya mbolea.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo kilele cha maadhimisho hayo itakuwa ni Oktoba 13 ambapo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe huku wadau mbalimbali wakitakiwa kujitokeza kwa wingi kuanzia siku hiyo kupata elimu kwa kuzingatia kuwa msimu wa kilimo unakaribia.

**Imeandaliwa na Halima Ikunji na Benny Kingson (TABORA).**

# Waomba kujengewa uzio wa shule kudhibiti uhalifu

**Na Timothy Itembe** TARIME

UONGOZI wa Shule ya Sekondari Tarime umeiomba serikali kwa kushirikiana na mamlaka zinazohusika pamoja na wadau mbalimbali kuwasaidia kujenga uzio katika shule hiyo, ili kuimarisha usalama na kudhibititi uhalifu kwa wanafunzi.

Ombi hilo limetolewa juzi na Mkuu wa Shule hiyo, Maro Chenge wakati akiongea Nipashe na kusema kuwa shule hiyo ipo katika mazingira hatarishi na usalama uliopo ni mdogo kutokana na kuwa wazi hali inayosabibisha mwingiliano wa mara kwa mara na watu kutoka nje ya shule.

"Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 kama shule yametusaidia kupata mradi wa maji ambao haukuwepo kwa miaka 50 iliyopita, sasa tuna maji kutoka Sekondari ya Bomani baada ya baraza kuagiza MUWASA kufanya hivyo," alisema Chenge.

Mkuu huyo alisema awali walikuwa wanatumia maji ya kisima cha kupampu na kuwa sensa ni kwa ajili ya mipango jumuishi na maendeleo endelevu ya nchi na yataongeza uwazi katika kugawa rasilimali zilizopo kuendana na uwiano wa idadi ya watu katika ngazi zote za utawala.

Hatua nyingine alisema utekelezaji wa mradi huo umesaidia watoto kupata muda wa kujisomea tofauti na hapo awali walipokuwa wanatumia muda mwingi kutafuta maji.

Hivyo waliiomba serikali na wadau mbalimbali kuwasaidia kumaliza changamoto ya uzio inayowakabili kwa sasa.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Musoma(MUWASA) Kanda ya Mara, Nicas Mugisha alisema changamoto ya upatikanaji maji katika mji wa Tarime bado ni kubwa.

"Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 Mji wa Tarime unakadiriwa kuwa na wakazi 133,043. Kwa wastani tunatoa huduma ya maji safi na salama kwa wakazi wapatao 69,981 (52.6%) ya watu waishio katika Mji wa Tarime, ambapo malengo ya MUWASA ni kufikisha 95% ya watu wote kupata huduma ya majisafi na salama.



Ukurasa 12

Christina RC anayehimiza faragha unyonyeshaji mtoto



Ukurasa 13

Historia ilivyomwandaa Kardinali, miaka 60 baada ya Rugambwa

Nipashe

# TESA

Jumanne Oktoba 10, 2023

TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 14

**Madaktari na walimu kusimamia miradi ujenzi ni kuvuruga utaalamu**

ELIMU

NA CHRISTINA MWAKANGALE

# Kutoajiri walimu kunavyopeleka kilio masomo ya sayansi, hesabu

• Upungufu chanzo maelfu sekondari kuambulia ziro



Wadau wa elimu, Dk. Athuman Mfutakamba (mwenye tai) na Nyambari Nyangwine (aliyevaa kofia), wakijumuika kufurahia Siku ya Walimu Duniani. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

OKTOBA 5, ni Siku ya Walimu Duniani, mwaka huu 'jambo la walimu' likifanyika kitaifa wilayani Bukombe mkoa wa Geita.

Walimu kutambulika, kuheshimika na kuthaminiwa ni lazima ili kufikia maendeleo endelevu, ndiyo maana Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu na Sayansi na Utamaduni UNESCO, linasema walimu milioni 44 wanahitajika, kutimiza lengo la kusambaza elimu ya msingi na sekondari kwa wote ifikapo 2030.

Hali ya walimu nchini ina vilio vingi kuanzia uchache wao, kazi ngumu hadi uhaba wa vitendeakazi. Ili kufahamu zaidi Nipashe, inazungumza na Naibu Waziri mstaafu, Dk. Athuman Mfutakamba, anayetaja changamoto kadhaa, zinazosababisha kushuka ufaulu nchini mzizi ukiwa ni matatizo ya walimu.

"Upungufu wa walimu ni mkubwa na kusababisha ufaulu duni miaka ya 2021 na 2022, nilifuatilia baadhi ya wabunge wakichangia Ripoti ya Kamati ya Maendeleo na Huduma za Jamii kipindi cha Januari 2022 hadi Januari 2023, chini ya Mwenyekiti Stanislaus Nyongo, mbunge wa Maswa Mashariki, anayekiri upungufu huo."

Aidha, katika sekondari za serikali umesababisha ufaulu duni kwa wahitimu wa kidato cha nne mwaka 2022 kwenye sayansi, hisabati na fizikia (STEM).

Moja ya sababu, anazozibaini ni upungufu wa ajira mpya kwa walimu wa masomo hayo tangu 2017 wakati idadi ya wanafunzi ikiongezeka, akisema mwaka jana, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ilipokea maombi 30,000 ya walimu wa sayansi lakini ili iliajiri 5,000 ili kufundisha shule za sekondari.

Anaitaka serikali kuangalia tatizo hilo, kwa kuwa lengo ni kufikia uchumi wa viwanda ifikapo 2025 kama inavyoelekeza Dira ya Maendeleo 2025, akisisitiza uwepo mikakati madhubuti inayolenga kuwa na msingi wa masomo ya STEM na jiografia.

"Viwanda na sekta binafsi ambayo ni mwajiri mkuu zinahitaji wataalam wanaozalishwa na STEM ili uchumi uendelee. Miaka michache iliyopita walimu 165,948 waliomba kazi lakini walioajiriwa ni 16, 000," anasema Dk. Mfutakamba.

Dokta Mfutakamba Naibu Waziri wa Uchukuzi mstaafu wa awamu ya nne, pia mbunge wa Igalula, anasema takwimu za sasa za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia zinataja mahitaji ya nchi ya walimu wa hisabati kuwa 19,216 lakini walioko kazini ni 5,537 sawa na asilimia 29 kisababisho cha wanafunzi kwa asilimia 83 kupata F kidato cha nne, mwaka 2022.

"Nchi inahitaji walimu wa fizikia 16,334 shule za sekondari, waliopo ni 3,758 sawa na asilimia 23. Hii imesababisha asilimia 82 ya wanafunzi wa kidato cha nne kupata ziro. Walimu wa kemia wanahitajika 16,664 na waliopo ni 6,074 sawa na asilimia 36.

"Mwaka 2022 wanafunzi kwa asilimia 67 walipata F somo hili. Kwenye baiolojia hitaji ni walimu 17,813, waliopo 5,795 sawa na asilimia 33. Mtihani wa taifa matokeo kidato cha nne asilimia 53 ya watahiniwa kupata F."

Anasema jiografia wanahitajika 18,181 waliopo 13,755, wanaopungua ni 4,526 hali iliyosababisha asilimia 45 ya wanafunzi kidato cha nne 2022 kupata ziro, akitaka kutatua changamoto hiyo kwa wakati."

### MFUKO WA MKOA

Anataja umuhimu wa kuanzisha mfuko wa kusaidia kupata walimu wa STEM kwa kila mkoa kwa kuangalia vyanzo mbalimbali kwa kuwa serikali bajeti kuu mahitaji yake ni mengi na inaangalia taifa zima.

"Mkoa unaweza kuwa na kamati ndogo inayofikiria mapendekezo na kuwasilisha kwa Mkuu wa Mkoa na kuona utekelezaji ili kuinua kiwango cha ufaulu wa masomo hayo," anashauri Dk. Mfutakamba.

Walimu Liberatha Alexanda na Vincent January, wanafundisha kwa kujitolea masomo ya sayansi shule ya sekondari Goba Mpakani, iliyopo Tegeta A, jijini Dar e Salaam, ambayo ina walimu 36 na wanafunzi 1,074 kati yao wasichana ni 564 lakini ina uhaba wa walimu wa masomo hayo.

"Nimemaliza mafunzo Chuo cha Ualimu Korogwe, mkoani Tanga, nikisomea hisabati, sayansi na kemia, Mei mwaka huu. Niliamua kujitolea shuleni hapa, ili niongeze ujuzi kabla ya kuajiriwa, baada ya kuona shuleni hapa mwalimu wa sayansi ni mmoja anafundisha kutoka kidato cha kwanza hadi cha nne. Anasema Liberatha.

Kadhalika, anaongeza kuwa katika masomo ya hisabati, baiolojia na fizikia mwalimu ni mmoja. Akaamua kuliko kukaa bure bora ajitolee na kuiomba serikali iangalie kwa jicho la pili na kwa kipaumbele wanaojitolea.

Mwalimu January anaeleza kuwa anajitolea shuleni hapo tangu ahitimu masomo yake ingawa changamoto ni kipato na anatumia muda wa ziada shuleni kufundisha wanafunzi jioni ili kujikimu.

**INAENDELEA UK.12**

ELIMU
NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Christina RC anayehimiza faragha unyonyeshaji mtoto

• Asisitiza kulindwa utu, heshima ya mwanamke



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, akikagua ujenzi wa soko kuu Manispaa ya Shinyanga, na kuagiza kijengwe chumba maalumu cha kinamama kuwanyonyeshea watoto.
**PICHA: MARCO MADUHU**

KINAMAMA wanakumbushwa kunyonyesha mtoto mchanga ndani ya saa moja mara wanapojifungua ili kumpa kinga ya maradhi, kumlinda dhidi ya maambukizi ya magonjwa ya masikio, njia za hewa na kuwaepusha na kuhara.

Shirika la Afya Duniani (WHO) linaelekeza kuwapa maziwa kwani hufyonzwa kwa wepesi na urahisi, hakuna kuvimbiwa, watoto wachanga wanakua na kuongezeka uzito kwa haraka zaidi na wanaimarika pale wanapolishwa maziwa ya mama pekee kwa miezi sita mfululizo bila kula chochote hata maji, na kitaalamu inathibitika kuwa wanakuwa na uwezo mkubwa wa akili (IQ).

Ndiyo maelezo ya kisayansi kwa wanawake na jamii na wadau wanapaswa kuwasaidia kinamama ili kuwapa watoto haki yao ya afya.

Christina Mndeme, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanya, anasema afya ya mtoto ni kila kitu, akiagiza wafanyabiashara masokoni wenye watoto wanaonyonya wajengewe vyumba vya faragha kwa ajili ya kunyonyesha na kufurahia na watoto wao.

Kwa Watanzania wengi kunyonyesha kunachukuliwa kama jambo la kawaida hata sokoni kinamama wengine hutoa matiti na kuwapa watoto hata mbele ya wateja sokoni au popote jambo ambalo linatafsiriwa kama ni udhalilishaji.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Christina, akiwa katika ziara ya kukagua ujenzi wa ukarabati soko kuu la Manispaa ya Shinyanga, anaagiza ufanyike usanifu wa kujengwa chumba maalumu ambacho kitakuwa cha faragha kwa ajili ya kunyonyesha watoto.

Anasema, masoko yote aliyoyatembelea mkoani humo , hajawahi kuona kuna chumba maalumu ambacho kimejengwa mahususi kwa ajili hiyo.

"Naagiza masoko yote Shinyanga ambayo yanaendelea kujengwa likiwamo soko kuu na soko la Ndala, kufanyike usanifu na kujengwa chumba cha faragha kwa ajili hiyo,"anaagiza Christina.

"Ni kitendo cha ajabu mama anamuuzia mteja wake bidhaa huku akinyonyesha hadharani siyo kitu kizuri lazima wawe na faragha na kujengewa chumba maalumu watakapocheza na kucheza watoto wao wakati wakiendelea na biashara,"anaongeza Mkuu wa Mkoa.

Anasisitiza kuwa maziwa ya mama ni chakula bora kwa mtoto kwani yana kiasi na kiwango sahihi cha virutubisho anavyohitaji, pia ni laini kwa tumbo lake linalokua pamoja na utumbo na mifumo mingine ya mwili. Inashauriwa kumnyonyesha hadi mtoto afikishe umri wa miezi sita kisha kumnyonyesha na kumpa vyakula vizito baadaye vigumu hadi mwaka mmoja na hata miwili.

Akishangia hatua hiyo, Ruth Joseph mfanyabiashara katika soko kuu Manispaa ya Shinyanga, anasema kina mama wa sokoni wanahitaji faragha ya unyonyeshaji, lakini kutokana na mazingira wamekuwa wakinyonyesha hivyo hivyo hata mbele ya wateja.

Analisifu wazo la Mkuu wa Mkoa akisema ni muhimu kwa sababu ya kutunza utu wao, hasa pale wanapotoa titi kunyonyeshamtoto huku wakiwahudumia wateja tena wanaume.

"Mfano upo na mteja wa kiume una mhudumia huku mtoto naye analia njaa anataka kunyonya utafanyaje, ukisema ukae umnyonyeshe kwanza mtoto mteja anaondoka, itabidi tu ufanye hivyo ili usikose hela yake,"anasema Ruth.

Sarah Richard anasema licha ya mteja wa kiume hata wafanyabiashara wenzao wa jinsi tofauti kutoa matiti mbele yao na kunyonyesha siyo jambo jema, bali inahitajika faragha na kutunza heshima ya mwanamke na mtoto wake.

Ofisa Lishe Manispaa ya Shinyanga Amani Mwakipesile, anasema unyonyeshaji watoto ni jambo la muhimu, sababu ya kuwajenga kiafya na kiakili na kuwaokoa na maradhi mbalimbali ikiwamo udumavu.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Dk.Yudas Ndungile, anasema unyonyeshaji watoto maziwa ya mama kwa miezi bila kuwalisha chochote, umesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo la udumavu kwa walio chini ya miaka mitano mkoani humo kutoka asilimia 32 mwaka 2018 hadi kufikia asilimia 27mwaka jana.

Anasema udumavu huo umepungua kutokana na kutoa elimu ya unyonyeshaji na lishe bora ambayo imekuwa ikitolewa kwa wazazi na walezi, na kueleza kwamba bado jitihada zinahitajika kuelimisha kinamama wakiwamo wafanyabiashara.

Kaimu Mhandisi wa Manispaa ya Shinyanga Kassimu Thadeo, akizungumzia utekelezaji wa agizo la Mkuu wa Mkoa kuhusu kwenye soko hilo, anasema usanifu wa soko kuu Manispaa ya Shinyanga, haukuwa na chumba cha faragha, lakini ujenzi unaendelea na kwamba watakijenga.

Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga Michael Makotwe, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Alexius Kagunze, anasema ujenzi wa soko hilo umefikia asilimia 57 na utakamilika Desemba mwaka huu, akieleza kuwa gharama yake ni bilioni 1.8 ambazo zimepatikana kwenye fedha za mapato ya ndani.

## Kutoajiri walimu kunavyopeleka kilio masomo ya sayansi, hesabu

**INATOKA UK.11**

Mbunge wa za mani wa Tarime (CCM), Nyambari Nyangwine ni mwalimu na mwandishi wa vitabu, anayesema:

"Walimu wanaojitolea wapewe kipaumbele kwenye ajira, inawezekana maofisa elimu hawajui kinachoendelea kwenye shule tofauti. Pia changamoto za walimu ni nyingi pamoja na kukosa mafunzo ya kuwajengea uwezo kama ambavyo watumishi wa sekta nyingine wanavyopatiwa."

Kadhalika, anaeleza kuwa vijijini walimu wanatembea umbali mrefu kwenda kufundisha na kushauri wajengewe makazi shuleni na kupewa vitendea kazi kufanikisha ujifunzaji na ufundishaji.

Kwenye maadhimisho ya siku ya walimu kitaifa , Naibu Waziri Mkuu Dk. Doto Biteko, akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan, huku akimpigia simu mubashara, Rais anaahidi kuwa serikali itaendelea kushughulikia changamoto za walimu hatua kwa hatua, ikiwa ni pamoja na kuwapandisha madaraja na kutoa malipo na stahiki mbalimbali.

"Walimu ni jeshi kubwa na serikali inathamini mchango mkubwa mnaoutoa, itaendelea kufanyia kazi changamoto zenu, ili hali zenu ziwe bora zaidi, hivyo nimemwagiza Naibu Waziri Mkuu, Dk. Biteko, awasikilize kisha aniletee maazimio mliyoyafikia ili niyafanyie kazi."

Wiki iliyopita serikali ilizindua mpango wa kutoa mikopo kwa wanafunzi 8,000 yenye thamani ya Shilingi bilioni 48, kwa kiwango cha masomo ya diploma kwa mwaka wa masomo 2023/24.

Fani zinazopewa kipaumbele ni pamoja na afya, sayansi, fizikia na hisabati lengo likiwa ni kuleta mageuzi katika sekta ya elimu.

ELIMU
NA GAUDENSIA MNGUMI

PROTASE RUGAMBWA

# Historia ilivyomwandaa kuwa kardinali, ni miaka 60 baada ya Lauren Rugambwa

• Wadau: Asaidie kukabili madhara tabianchi, njaa


IJUMAA Oktoba 6, ilikuwa ni siku ya shangwe, vifijo na nderemo ya mapokezi na kumkaribisha nyumbani Kardinali Protase Rugambwa, mwanadiplomasia na kiongozi wa kanisa aliyepewa wadhifa wa ukardinali hivi karibun Jijini Vatican .

Waumini mbalimbali wakiungana na Wakatoliki, wakazi wa Dar es Salaam wanaoongozwa na Makamu wa Rais Dk. Phillip Mpango, wanakusanyika uwanja wa ndege wa Julius Nyerere Dar es Salaam kumlaki kiongozi huyo wa kiroho.

Alikuwa akirejea nyumbani kutoka Roma Italia, baada ya kupewa wadhifa wa ukardinali, mlango wa ndege unapofunguliwa saa 8:00 mchana, Kardinali Protase Rugambwa, ndani ya zulia jekundu, analakiwa na Makamu wa Rais. Akiwa na miaka 63 anaandika historia mpya Tanzania kuwa kardinali wa tatu, anayekwenda kufanya kazi ya kichungaji Jimbo Kuu Katoliki Tabora.

Makardinali waliomtangulia ni wa kwanza Mwafrika Laurian Rugambwa (marehemu), aliyepewa jukumu hilo miaka ya 1960, akifuatiwa na Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo, sasa mstaafu.

Kardinali Rugambwa amerejea nchini baada ya kufanya kazi za kichungaji na kitume huko Roma akilitumikia Kanisa 2012 hadi Septemba mwaka huu, katika Shirika la The Pontifical Mission Societies (PMS).



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akimkaribisha Kardinal Protase Rugambwa. **PICHA: TEC**

**NYOTA ILIPOWAKA**

Wakati wa kusanyiko la kumsubiri uwanja wa ndege, waumini wanazungumza mengi kuhusu Kardinali Rugambwa, mojawapo ni kuwa alizaliwa kimiujiza, mama yake alibeba ujauzito wake kwa muda wa miezi 11 na siku ya kuzaliwa kwake, ndiko Kardinali Laurian Rugambwa aliporejea nchini kutoka Roma.

Nipashe inamuuliza swali hilo, Padri Florence Rutaihwa, Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Kichungaji, Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), kwanza, iwapo Kardinal Protase Rugambwa, ana uhusiano na Kardinal Laurean Rugambwa?

Padri Rutaihwa, anajibu kuwa hawana uhusiano wala nasaba, isipokuwa alipewa jina kwa heshima ya Kardinal Laurean Rugambwa, ambaye siku anaporejea Tanzania Mei 31, 1960 baada ya kupewa wadhifa wa kuwa Kardinali huko Roma, ndiyo siku alipozaliwa Mwadhama Protase.

Anafafanua kuwa alipewa jina hilo na mjomba wake aliyekuwa rafiki wa Mwadhama Laurean, ambaye alikwenda kumpokea, kumpongeza na kumkaribisha na kwa furaha ya kusherehekea dada yake kupata mtoto siku hiyo , akampa jina hilo, hivyo hawana uhusiano.

Aidha, anaeleza kuwa zipo taarifa kuwa mtumishi huyo wa Mungu inawezekana alichukuliwa mimba kwa muda mrefu takribani miezi 11 na kwamba watu wanasema alichelewa sana kuzaliwa.

Akifafanua zaidi anasema kwa Kihaya, Rugambwa maana yake ni mtu anayezungumziwa na kusifiwa kwa mema na anayependwa kwa mambo mazuri na ya mfano anayo au aliyoyafanya.

Akizungumzia utumishi Vatican, anasema alikuwa PMS shirika la Kipapa ( Baba Mtakatifu) linalohusisha marafiki wa Papa wanaoshughulikia kutoa misaada na kusaidia mashirika ya kanisa kwenye majimbo kote dunia.

"Misaada huelekezwa kwenye mambo ya kijamii ikiwamo mafunzo na elimu kupitia mashirika yanayotangaza Injili katika mataifa mbalimbali ," anasema.

Kiongozi huyo ambaye ni Askofu Mkuu Mwandamizi, alianzia kazi mkoani Tabora akiwa Askofu wa Jimbo, na anapowasili, anapokea pongezi na salamu za Makamu wa Rais Dk. Mpango, anayesema uteuzi wake ni sifa kwa Tanzania na kuahidi kushirikiana na kanisa kuleta amani na maendeleo .

"Kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais anamkaribisha nchini akimwambia mwanadiplomasia huyo kuwa uteuzi wake ni baraka kwa taifa na hata alipokuwa Vatican amekuwa akizungumzia na kuiombea Tanzania iwe yenye amani na mafanikio."

**MAPOKEZI BARAZA LA MAASKOFU**

Anapokaribishwa na viongozi wa Kanisa Katoliki makao makuu ya Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Kurasini, Mwadhama Kardinal Protase, anaanza jukumu lake kwa kulibariki kusanyiko la waamini na marafiki kwenye kanisa dogo la TEC anapolakiwa kwa furaha.

Anakaribishwa kwa sala fupi, nyimbo za kumsifu Mungu naye akizunguka kanisa zima kuwabariki waliokusanyika kumkaribisha nyumbani, anaowaambia amepokea kazi yake kwa heshima na unyenyekevu mkubwa na ataifanya kwa upendo na bidii kama ambavyo Mungu amempa jukumu la kulitumikia kanisa na taifa.

> Kardinali Rugambwa amerejea nchini baada ya kufanya kazi za kichungaji na kitume huko Roma akilitumikia Kanisa 2012 hadi Septemba mwaka huu, katika Shirika la The Pontifical Mission Societies (PMS).

Akiwashukuru Watanzania pote duniani, anasema mwishoni mwa mwezi uliopita, Papa Fransisko, aliwapa wadhifa wa kuwa makardinali maaskofu wakuu 21 na jina lake liliposikika Watanzania wanaoishi Italia kwa umoja wao walikusanyika kumshangilia, kumpongeza na kumwombea mafanikio katika jukumu hilo lenye heshima.

"Bila kujali dini wala imani zao tulikaa pamoja wakanipongeza na kusherehekea," anasema kiongozi huyo ambaye ni mnyenyekevu na mwenye furaha muda wote.

Kardinali Rugambwa, anapoingia TEC, anashangiliwa na maaskofu, mapadri, watawa, waseminari na vyama mbalimbali vya kitume vya Kanisa Katoliki, mabalozi na wawakilishi kutoka nchi mbalimbali duniani,anaowaeleza kuwa safari yake ya kutangaza Injili, imepata baraka na maombi kutoka kwa viongozi akimtaja Kardinal Pengo.

Anagusia, utabiri wake akisema Mwadhama Pengo alimtabiria mambo makubwa na sasa anayaona yakitimia na kutaka watu wazidi kumwombea pamoja na kanisa ili afanye kazi aliyokabidhiwa kwa upendo, uaminifu akitimiza mapenzi ya Mungu.

Akijibu hoja Mwadhama Kardinali Pengo, ananukuu Injili ya Luka 2:29... "Sasa Bwana umetimiza ahadi yake umruhusu mtumishi wako apumzike ...," ombi lililoufanya umati kulipuka kwa shangwe.

Kazi ya makardinali ni kumshauri Papa maeneo mbalimbali atakayohitaji, aidha, ni jopo la makardinali linalomchagua Baba Mtakatifu (Papa) iwapo atastaafu, kuumwa au kufariki dunia jopo hilo likiitwa 'Conclave' ambao ni mkutano wa faragha au wa siri kubwa unaohusisha makardinali pekee.

INAENDELEA UK.14

ELIMU

NA REUBENI LUMBAGALA, DODOMA

# Madaktari na walimu kusimamia miradi ujenzi ni kuvuruga utaalam

MOJA ya mafanikio ya utekelezaji wa sera ya elimumsingi bila ada iliyoanza mwaka 2016 ni ongezeko kubwa la wanafunzi katika ngazi zote za elimu kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu.

Kuongezeka huko kunatokana na uamuzi wa serikali wa kutoa ruzuku (capitations) kugharamia elimu ya awali hadi kidato cha sita ili wanafunzi wapate haki yao ya msingi ya kusoma bila kikwazo na hatimaye kujenga jamii yenye maarifa, ujuzi na stadi muhimu kwa ajili ya kumudu kuendesha maisha yao.

Kutokana na ongezeko la uandikishaji wanafunzi, ubora wa elimu inayotolewa ni lazima uzingatiwe , aidha, ubora wa elimu inayotolewa uende sambamba na uboreshaji na ujenzi wa miundombinu bora ya elimu.

Miundombinu hiyo ni madarasa, kumbi za mihadhara, mabweni, mabwalo, ofisi za walimu, maabara za sayansi na lugha, maktaba, vyoo, nyumba za walimu na vyumba vya TEHAMA ili wanafunzi waweze kupata elimu bora inayokwenda sambamba na maendeleo ya sayansi na teknolojia yaliyopo ndani na nje ya nchi.

Ongezeko kubwa la wanafunzi katika taasisi za elimu, umepelekea kila mwaka serikali kupeleka fedha katika halmashauri na fedha hizo kuingizwa moja kwa moja katika akaunti za shule za msingi na sekondari ili kutumiwa kuboresha miundombinu ya elimu katika shule hizo.

Ili kutimiza azma ya serikali ya kuboresha na kujenga miundombinu bora, inasisitiza ulazima fedha hizo zisimamiwe kikamilifu ili thamani ya fedha iweze kuonekana kupitia miundombinu itakayojengwa.

Changamoto inayotajwa sasa ni walimu kupewa jukumu la kusimamia ujenzi wa miundombinu hiyo wakishirikiana na kamati na bodi za shule.



Sehemu ya majengo ya Chuo Kikuu cha Dodoma. **PICHA: UDOM**

Pamoja na uongozi wa shule kushirikiana na watumishi wengine wa halmashauri kama vile wahandishi, ofisi ya manunuzi, mipango na elimu, ila wasimamizi wakubwa ni walimu wenyewe kupitia kamati zilizoundwa na shule zao.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora George Simbachawene, akiwa katika ziara ya kukagua ujenzi wa vyumba viwili vya maabara katika Shule ya Sekondari Rudi iliyopo Kibakwe, mkoani Dodoma, anatoa rai kuwa madaktari na walimu wasisimamie miradi ya ujenzi katika maeneo yao ya kazi.

Anawaambia kuwa usimamizi wa ujenzi si taaluma yao na kuwatumia ni matumizi mabaya ya rasilimaliwatu.

"Kwa sasa majengo yetu yanajengwa na walimu na madaktari badala ya wahandisi wa ujenzi, hii haukubaliki halmashauri ajirini wataalamu wa ujenzi hata kwa ajira ya mkataba ili waweze kusimamia ujenzi," anasema.

Anaongeza kuwa haiwezekani miradi hiyo isimamiwe na walimu na madaktari kwani kitaaluma sio wahandisi wa majengo wala ujenzi.

Anakumbusha kuwa miradi hiyo ya ujenzi inayotekelezwa inagharimu fedha nyingi ambazo thamani yake ni lazima ionekane na vilevile, ujenzi huo ni lazima uwe na ubora ili miundombinu hiyo ya elimu na afya idumu kwa muda mrefu zaidi.

Kwahiyo, ni muhimu kuwatumia wahandisi wenye taaluma ya ujenzi ili miradi ya afya na elimu iwe bora, Waziri Simbachawene anaongeza akisema kuwa imekuwa ni jambo la kawaida kama mradi wa afya unatekelezwa basi msimamizi wa ujenzi atakuwa daktari, vivyo hivyo kama ujenzi wa madarasa basi msimamzi atakuwa mwalimu.

Rai ya Waziri Simbachawene ni kuwa utaratibu huu uangaliwe ili miradi ya afya na ujenzi iwe bora, akitambua kuwa walimu wanatoa elimu bora ili kuongeza ufaulu katika shule zao. Akieleza kuwa kuwatumia walimu katika shughuli za ujenzi kunawaathiri katika utekelezaji wa majukumu yao ya msingi ya kufundisha darasani.

Kadhalika madakatari kwa upande wao, wanao wajibu wa kuwahudumia wagonjwa hospitalini ili kutatua kero za kiafya, kupewa jukumu jingine la usimamizi wa majengo kunaathiri utekelezaji wa majukumu yao ya msingi ya kuwahudumia wagonjwa.

Taaluma za ualimu na udaktari ni nyeti katika jamii na taifa, kadhalika uhandisi nao, walimu na matabibu wanapaswa kutumia muda wao katika kutimiza majukumu yao ya kuwahudumia wanafunzi na wagonjwa ili kujenga jamii bora.

Ni watu wenye afya timamu na elimu ambao hawasumbuliwi na maadui ujinga, maradhi na umaskini.,

Aidha, katika utekelezaji wa majukumu hayo kuwatumia wahandisi katika ujenzi wa majengo ya elimu na afya kutapunguza hoja za kiukaguzi kutoka timu ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) na hata TAKUKURU.

Timu hizo ndizo zinazokagua miradi ya ujenzi katika halmashauri mbalimbali nchini na TAKUKURU inaweza kuhusika iwapo kuna mwenendo wa kuwapo rushwa.

Kwa ujumla wahandisi ndiyo wataalamu katika shughuli za ujenzi na si walimu na madaktari wanaosubiriwa darasani na wodini kutoa huduma kwa wananchi. Hoja ya Waziri Simbachawene ifikishwe maeneo mengine na ifanyiwe kazi kama kuna upungufu ufanyiwe kazi.

***Mwandishi ni Mwalimu wa Sekondari Mlali mkoani Dodoma.***

***Maoni: 0620 800 462.***

## Ubunifu kuvuna asali ulivyonusuru nyuki, wafugaji na kuokoa misitu

**INATOKA UK.13**

**MADHEHEBU YAMKARIBISHA**

Askofu William Mwamalanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Maaskofu na Mashekhe ya Maadili Amani na Haki za Binadamu kwa Jamii ya Madhehebu ya Dini, anapozungumzia uteuzi na makaribisho yake nchini anaanza kumpongeza Mwadhama Kardinal Rugambwa.

Anasema "Tunaungana naye kumshukuru Mungu kwa kupewa majukumu makubwa ya kikardinali, tunaona fahari kwa Tanzania tukiamini kwamba atakuwa nguzo kubwa ya kuunganisha viongozi wa dini nchini, Afrika na dunia pia," anasema.

Anasema kwa kuwa majukumu yake ni kumshauri Papa, ana wajibu wa kuzungumzia mambo yanayowaumiza Watanzania na Waafrika pia, akitaja suala la amani duniani kuwa ni muhimu kuungana ili kuwa na amani na maendeleo.

Askofu Mwamalanga, anataja njaa, akisema duniani kuna uhaba wa chakula na lakini Afrika ina shida, akimshauri kutumia diplomasia , uzoefu ,elimu na utume wa Kanisa kushauri na kupata chakula kwa kila mmoja.

"Tanzania ina ardhi, maji, watu na amani lakini taifa halijaweza kutumia ardhi na maji kupata chakula cha kutosha. Aidha, hakuna maji safi na salama kwa ajili ya watu mijini na vijijini."

Anamtaka kushauri na kushirikiana na serikali kupata ufumbuzi kwa kuwa kanisa linaamini kuwa huwezi kufanikisha utume na uinjilishaji wa roho peke bila mwili ambao ni kuwapo amani, chakula, kilimo, ufugaji, maji na mendeleo ya jamii nzima ambayo hakuna anayeachwa nyuma.

Anakumbusha mabadiliko ya tabianchi, akisema:"Kardinali Rugambwa ni mwanadiplomasia mkubwa wa kanisa, ameishi Ulaya anafahamu athari na mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi tunamuomba asaidie kupata uamsho mpya kwa kanisa, serikali na dunia kulishinda tatizo hili ili tuweze kuwa na Tanzania bora."





# M/kiti CCM ashtushwa kukithiri migogoro Ikungi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
IKUNGI

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Singida kimeshtushwa na migogoro mbalimbali inayoendelea katika Kata ya Ntuntu Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ambayo imesababisha wenyeviti wanne wa serikali za vijiji kutimuliwa kwenye uongozi.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Singida, Martha Mlata, akizungumza na wajumbe wa mkutano mkuu wa wilaya hiyo katika ziara yake alisema wananchi na viongozi wanatakiwa kuondoa migogoro na tofauti zao ili kukiimarisha chama.

Alisema, migogoro haitakiwa ndani ya chama na kuwataka viongozi wa CCM Wilaya ya Ikungi kuwa wamoja ili kusimamia miradi ya maendeleo ambayo serikali imeendelea kutoa mamilioni ya fedha kuitekeleza.

Mlata alisema viongozi na wananchi wanapaswa kusimama imara kumtetea Rais Samia Suluhu Hassan, pale inapotokea baadhi ya watu wanamsema vibaya.

Naye Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa kutoka Mkoa wa Singida (MNEC), Yohana Msita alisema kuwa chama hicho hakitamvumilia kiongozi yeyote aliyewekwa madarakani na CCM kama atakuwa anakiuka taratibu za chama na serikali.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Ally Mwanga aliishukuru serikali kwa kuendelea kutoa fedha nyingi kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika Wilaya ya Ikungi.

Mwanga alisema kuwa kupitia mradi hiyo inayotekelezwa na serikali imesaidia kupunguza changamoto za wananchi kufuata huduma za kijamii mbali na maeneo yao.

Naye, Mjumbe wa Kamati ya Siasa Mkoa wa Singida, Denis Nyiraha, alisema kuwa lengo la CCM ni kushinda chaguzi zote zitakazofanyika nchini na kuwataka wanachama na viongozi kushirikiana ili kukiimarisha chama.

# Askofu aonya vitendo vya ushirikina katika uchaguzi

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

ASKOFU wa Mkuu wa Kanisa la Pentekostal Christian Internation, Thomas Kiula, amewaonya viongozi watakaogombea katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2024, kutojiingiza kwenye imani za ushirikina badala yake wamuombe Mungu ili awape kibali cha kuongoza.

Alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa akizungumza na waumini toka madhehebu mbalimbali ya dini, kwenye ibada ya kumsimika Mchungaji Henry Masinyulo iliyoambatana na uzinduzi wa jengo la kuabudia iliyofanyika katika Kanisa la Pentekostal Christian Internation (P.C.I) lililopo Mtaa wa Ndachi Kaya ya Mnadani Jiji la Dodoma.

Mchungaji Kiula alisema tabia ya kujishirikisha na ushirikina kwa waganga wa kienyeji kunasababisha kupata viongozi wabovu wasio mcha Mungu.

"Hawa wanaokimbilia kwa waganga wanasababisha tuwe na viongozi wanaojali maslahi yao binafsi badala ya kuwatumikia watu waliomchagua," alisema.

Naye, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tawi la Amani Kata ya Mnadani, Mussa Mgonela aliwataka vijana kuunga mkono juhudi zinazofanywa na serikali kwa kufanya kazi kwa vitendo, huku wakibuni mbinu mbalimbali za miradi badala ya kukaa na kusubiri ajira.

Akizungumza kwenye ibada hiyo kwa niaba ya Diwani wa Kata ya Mnadani, Paul Bankie alisema vijana wanapaswa kushiriki kwenye shughuli mbalimbali za kimaendeleo kama vile ya kilimo, ufugaji, uvuvi.

Mchungaji Henry Masunyilo wa kanisa hilo la Pentecostal Christian International Ndachi akitoa shukrani baada ya kusimikwa akiwahimiza Watanzania kuungana kwa pamoja katika kuliombea Taifa.



Wananchi wakipita kwa nafasi kwenye Mtaa wa One Way jijini Dodoma jana, baada ya uongozi wa Jiji hilo kuwaondoa wafanyabiashara wadogo (Machinga) waliokuwa wanaziba barabara hiyo na kusababisha msongamano. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Diwani matatani kuchelewesha ujenzi wa majosho

**Na Thobias Mwanakatwe,**
IRAMBA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kumhoji Diwani wa Kata ya Tulya katika Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Wilfred Kizanga, kuhusu kutokamilisha ujenzi wa majosho matano kwa wakati.

Pia, amemwagiza Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda, kukiandikia barua Chama Cha Mapinduzi (CCM) kumshtaki diwani huyo kwa uhujumu uchumi na taarifa azipate ofisini kwake.

Alitoa maagizo hayo juzi baada ya kufanya ziara wilayani hapa na kupewa taarifa ya miradi ya maendeleo iliyojengwa kwa fedha za serikali katika mwaka wa fedha wa 2022/23 ambayo haijakamilika.

Serukamba alisema Sh. milioni 125 zilitolewa kwa ajili ya kujenga majosho hayo ambayo yalipaswa kukamilika Mei 30 mwaka huu kabla ya mwaka mpya wa fedha 2023/24 kuanza, lakini haijakamilika na fedha alishalipwa mkandarasi huyo.

Alisema diwani huyo ambaye ni mmiliki wa Kampuni ya DHR, anapaswa kuandika maelezo kwa maandishi TAKUKURU kuwa lini atakamilisha miradi hiyo ambayo imechukua muda mrefu bila kukamilika.

Naye Ofisa Mifugo wilayani Iramba, Dk. Dotto Peter, alimweleza Serukamba kuwa serikali ilitoa fedha hizo kwa ajili ya kujenga majosho hayo katika vijiji vya Maluga, Kinampanda, Mtoa, Shelui na Ndulungu na hayajakamilika kuchomelewa vyuma eneo la mzunguko.

Alipoulizwa kwanini majosho ya Kinampanda, Mtoa, Ndulungu na Shelui hakuna umeme kama Maluga, Dk.Peter alisema kila josho lina sababu yake ambazo pia hakuzifafanua ni zipi lakini akaomba mkandarasi apewe muda zaidi kukamilisha ujenzi.

Awali Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda, alisema baadhi ya watendaji wa wilayani hapa wanashindwa kuwa wakweli kwa sababu awali alipotembelea majosho hayo aliagiza mkandarasi anyang'anywe miradi kutokana na kuwa hawezi kuitekeleza kwa wakati.

# Serikali, Hellen Keller wajadili uimarishaji lishe katika familia

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

KATIBU Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Dk. Jim Yonazi amekutana na wadau wa maendeleo wa Shirika Hellen Keller Tanzania kwa ajili ya kujadili suala la kuimarisha sekta ya lishe kuanzia ngazi ya familia.

Akizungumza katika kikao hicho jana jijini hapa, Dk. Yonazi alisema sekta ya lishe inapaswa kupewa kipaumbele kwa sababu tunajenga taifa la kesho ili kuja kupata viongozi bora wa hapo baadae.

Alisema Ofisi ya Waziri Mkuu itaendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo kuhakikisha afua za lishe zinaboreshwa kwa wananchi kuhamasishwa kula vyakula vyenye virutubisho kwa kuzingatia mazingira yao yanayowazunguka.

Alisema, pamoja na wananchi kupewa elimu ya magonjwa yasiyopewa kipaumbele ili kujikinga kwa ustawi wa taifa bado serikali inaendelea kuhakikisha suala la lishe linasimamiwa kwa ukaribu katika kila hatua.

Alisema ipo haja ya kushirikiana pamoja kuhakikisha wananchi wanabadilisha fikra za jamii kuhusu masuala ya lishe na magonjwa kwa sababu itawasaidia kuacha kuishi kwa mazoea na badala yake wazingatie umuhimu wa kutunza afya zao ili waendelee kuwa sehemu ya uzalishaji katika familia zao na Nchi kwa ujumla.

Dk. Yonazi alisema suala la lishe likizingatiwa taifa litakuwa bora kwa sababu jamii hususani watoto watakuwa katika afya bora kutokana na kupata vyakula vyenye lishe.

Naye, Mkurugenzi wa Shirika la Helen Keller Tanzania, Dk. Degratius Ngoma alieleza kwamba jukumu lao kubwa ni kujenga uelewa kwa jamii kuhusu vyakula hatarishi vinavyosababisha magonjwa yasiyoambukiza.

Alisema wamekuwa mstari wa mbele kuhakikisha jamii inapata elimu hiyo ikiwemo kuitumia kwa vitendo katika mazingira yanayowazunguka kwenye maeneo mbalimbali.

Alisema wanaishukuru serikali kutokana na ushirikiano wao wanaotoa kwenye suala la utekelezaji wa masuala ya lishe katika jamii mbalimbali hapa nchini.

Mtaalam na Mshauri wa Masuala ya lishe Dk. Theresia Jumbe kutoka shirika hilo alibainisha kuwa maazimio waliyofikia ni kuendeleza shughuli za uratibu wa masuala ya lishe katika kusimamia na kuchangia utekelezaji wa afua za lishe zilizoainishwa katika mpango jumuishi wa lishe (NMMNAP).





# Ukosefu vifaa wakwamisha jengo la upasuaji kutumika

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

LICHA ya ujenzi wa jengo la upasuaji la Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya kukamilika kwa zaidi ya miezi mitatu lakini bado halitumiki kutokana na kukosa vifaa.

Hali hiyo imeleza kusababisha msongamano wa wagonjwa kwenye Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya.

Aidha, katika hospitali hiyo ujenzi wa wodi ya wanaume umekamilika lakini halitumiki kutokana na kukosekana kwa vifaa vikiwemo vitanda hali ambayo inasababisha msongamano kwenye jengo dogo.

Hayo yalibainika juzi wakati wa ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera kwenye hospitali hiyo, iliyokuwa na lengo la kukagua ujenzi wa miundombinu mbalimbali iliyojengwa kwa zaidi ya Sh. bilioni saba.

Homera alibaini kuwa kati ya majengo matatu ambayo yamejengwa na kukamilika ni moja pekee ndilo linatumika ambalo ni jengo la mionzi lakini majengo hayo mawili yakiwa hayatumiki.

Homera alitoa siku 30 kwa viongozi wa hospitali hiyo kuanza kuyatumia majengo hayo, huku akimtaka mkandarasi aliyeyajenga kufanya marekebisho kwenye maeneo yenye dosari ndani ya wiki tatu pamoja na kuingiza maji.

Pia, aliagiza hospitali hiyo kuanza kutumia mapato yake ya ndani kununua baadhi ya vifaa wakati wakisubiri utekelezaji wa bajeti ya serikali ili kuharakisha huduma.

"Lakini pia mkikuta vitu haviendi vizuri, wasilianeni na Katibu Tawala wa Mkoa ili awasaidie kuwasiliana na Waziri wa Afya mpate vifaa hivi kwa dharura," alisema Homera.

Vilevile, aliwataka kutenga bajeti kwa ajili ya kuboresha mazingira ya hospitali hiyo ikiwa ni pamoja na kupanda maua na kuboresha njia za watembea kwa miguu.

Daktari Bingwa wa Uchunguzi na Tiba kwa kutumia mionzi wa hospitali hiyo, Dk. Mbwilo Mwakyusa alisema walipokea mashine ya uchunguzi wa magonjwa kwa kutumia mionzi (CT-Scan) Machi mwaka huu na wakaanza kuifanyia majaribio Aprili.

Alisema mpaka sasa wameshawahudumia wagonjwa zaidi ya 300 kwa kutumia mashine hiyo ambao baadhi yao wanatibiwa kwa kutumia bima ya afya na wengine wanalipa fedha taslimu.

Alisema kwa sasa wagonjwa wote wanaohitaji kipimo hicho wanapata huduma katika hospitali hiyo na kwamba imesaidia kupunguza msongamano kwenye hospitali ya kanda.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Hospitali hiyo, Dk. Julius Kaijage aliishukuru serikali kwa kuendelea kuboresha miundombinu ya hospitali hiyo ikiwemo ujenzi wa majengo na ununuzi wa vifaa.

Aliwataka watumishi wa hospitali hiyo kuitumia miundombinu hiyo vizuri katika kutoa huduma kwa wananchi na kuhakikisha wanavitunza vifaa ili vitumike kwa muda mrefu.



Naibu Katibu Mkuu wa CCM Bara, Anamringi Macha, akinyanyua picha ya Mwenyekiti wa Chama Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan baada ya kukabidhiwa na uongozi wa Shule ya Sekondari ya Jumuiya ya Wazazi Ivumwe jijini Mbeya, wakati wa harambee ya ujenzi wa vyumba vya madarasa iliyofanyika mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi, Gilbert Kalima na kulia ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu Taifa, Ndele Mwaselela. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## EWURA yawaita Watanzania wenye malalamiko

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma ya Nishati na Maji (EWURA) imewataka wananchi kuwasilisha malalamiko yao yanayohusu huduma hizo ili zitatuliwe mapema.

Ofisa wa Huduma wa EWURA, Francis Mhina aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa maadhimisho ya kilele cha wiki ya huduma kwa wateja.

Alisema mamlaka hiyo ndiyo iliyopewa dhamana ya kusimamia huduma hizo.

Mhina alisema malalamiko yakifikishwa kwenye ofisi za mamlaka hiyo kuna kitengo maalumu ambacho kipo kwa ajili ya kuyashughulikia ili kuhakikisha pande zote mbili zinanufaika.

"EWURA ilianzishwa kwa mujibu wa sheria na ndicho chombo cha kisheria ambacho kinasimamia taasisi zote zinazotoa huduma za nishati na maji, malalamiko yanayohusu mafuta, maji, gesi na hata umeme wananchi wanatakiwa kutuletea sisi," alisema Mhina.

Baadhi ya wadau wa mamlaka hiyo walisema EWURA ni chombo ambacho kinasaidia pande zote mbili ambazo ni mtoa huduma na mteja na hivyo malalamiko yanayotakiwa kufikishwa ni yale ambayo yameshindikana kutatuliwa kwenye hatua za awali.

Mwakilishi wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO), Ally Mwakula ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Madeni alisema wana kitengo cha kusikiliza kero za wateja na kutatua ili kupunguza malalamiko yanayopelekwa EWURA.

"Sisi tunaamini kwamba malalamiko yanayofikishwa EWURA ni yale ambayo tumeshindwa kabisa kusuluhishana kwenye ngazi ya taasisi zetu, lakini kuna baadhi ya wateja wanaleta hata malalamiko madogo, kwahiyo lazima tueleweshane," alisema Mwakula.

Alisema wataendelea kutoa elimu kwa wateja kuhusu namna ya kupata huduma mbalimbali ili kuepusha malalamiko ya kawaida kupelekwa EWURA.

# Njombe watenga ekari 80,000 kwa ajili ya uwekezaji

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, limekubali kutoa eneo la ekari 80,000 kwa ajili ya wawekezaji kutoka ndani na nje ya Mkoa wa Njombe watakaokuwa tayari kuwekeza katika kilimo cha maparachichi na mazao mengine ya matunda na mboga.

Eneo hilo ambalo lipo katika Kijiji cha Ikang'asi limepimwa afya ya udongo na wataalamu kutoka Wizara ya Kilimo na kubainika kuwa linafaa kwa kilimo cha mazao hayo.

Akizungumza katika kikao maalum cha baraza la madiwani la halmashauri hiyo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Valentino Hongoli alisema wananchi wapo tayari kuupokea mradi huo tangu ulipotambulishwa katika mkutano wa Kijiji cha Ikang'asi ambao ulifanyika Agosti 13 mwaka huu.

Alisema jambo kubwa madiwani wanapofanya mikutano na wananchi wao ni vizuri wakaendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa mradi huo wa uwekezaji wa kilimo kijijini hapo.

Alisema mradi huo una manufaa makubwa kwa wananchi wa Njombe, hivyo serikali inatakiwa kuharakisha utekelezaji wake mara moja ili matunda yaanze kuonekana.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, aliwatoa hofu madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kuwa eneo hilo la uwekezaji halitouzwa bali litaendelea kuwa ardhi ya wananchi wa Kijiji cha Ikang'asi.

Alisema yapo majina ambayo yanasambaa mitandaoni yakionyesha kuwa wameuziwa ardhi katika kijiji hicho habari ambazo hazina ukweli wowote.

Alisema wanachokifanya kwasasa watu hao ni kusaidia kutangaza shamba lililopo kwenye kijiji hicho ambacho kuna shamba limetengwa kwa ajili ya uwekezaji katika kilimo.

Alisema hata baraza hilo la madiwani linaweza kukaa na kujadili namna watakavyoona inafaa ili kuingia katika mradi huo wa uwekezaji katika kilimo Kijiji cha Ikang'asi ili mradi tu wafuate utaratibu.

Alisema mradi huo wa uwekezaji wa kilimo utakapotangazwa wananchi wanaruhusiwa kuomba na taratibu za malipo zitaelezwa hapo baadae.

Alisema, wamiliki wa ardhi katika mradi huo watakuwa wananchi wa Kijiji cha Ikang'asi, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe pamoja na Wizara ya Kilimo lengo ni kuzuia uuzaji holela wa eneo hilo.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi Utawala wa Ardhi, Hellen Philip aliwapongeza wananchi wa Kijiji cha Ikang'asi kwa kuitunza ardhi hiyo bila ya kuivamia na kuiharibu kwani sasa inakwenda kuwaletea fedha.

Diwani wa Kata ya Mfriga, Vasco Mgunda alisema mkakati wa uwekezaji wa kilimo katika kijiji hicho ulianza muda mrefu na hata alipochaguliwa kuwa diwani mwaka 2015 alianza kupambana ili uwekezaji huo uanze na wananchi wa kijiji hicho waweze kunufaika.



## Wanahabari Afrika kukutana Zanzibar kujadili TEHAMA

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUTANO Mkuu wa mwaka wa Umoja wa Mashirika ya Utangazaji wa Umma Kusini mwa Afrika kufanyika leo visiwani Zanzibar, ambapo Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi ataufungua.

Mkutano huo utakaodumu kwa muda wa siku tatu utashirikisha wakuu wa vyombo vya habari vya umma, wadau wa TEHAMA na wanahabari zaidi ya 200 kutoka nchi wanachama Kusini mwa Afrika na nchi nyingine za Afrika na duniani.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari, Rais wa umoja huo Stanley Benjamin Similo, alisema mkutano huo ni fursa adhimu kwa Afrika kwa sababu utazungumzia masuala ya TEHAMA katika kukuza teknolojia ya habari na utangazaji.

Aidha, alisema mkutano huo pia utajadili kwa kina nafasi ya TEHAMA na mchango wake katika ukuaji wa uchumi wa kidijitali Afrika ili kuleta maendeleo endelevu na kuonesha maboresho makubwa yaliyofanyika katika teknolojia ya habari.

Alisema zipo changamoto nyingi zinazokabili vyombo vya habari vya umma na hata watafiti wameonesha wafatiliaji wa maudhui ya vyombo vya habari vya umma zamani wanazidi kupungua na wanakimbilia kwenye mitandao kwa sababu ya kukuwa kwa teknolojia.

Naye Mkurugenzi wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Ayoub Rioba Chacha, alisema huo ni mkutano wa tatu kufanyika Tanzania kati ya nchi 16 za jumuiya hiyo na kwa mara ya kwanza utafanyika Zanzibar na ni nchi pekee zenye alama ambazo zimeungana.

Alisema: "Zanzibar pia ni moja ya maeneo muhimu ya utalii katika nchi kwani wageni watatembelea vivutio mbalimbali vya utalii vilivyokuwepo na kujionea uzuri wa pekee wa eneo hilo la nchi".

# Mfumuko wa bei ya vyakula visiwani Zanzibar wapanda

**Na Rahma Suleiman**
ZANZIBAR

MFUMUKO wa bei wa vyakula visiwani Zanzibar umepanda na kufikia asilimia 7.45 kwa kipindi cha Septemba kutoka asilimia 6.82 uliokuwa Agost mwaka huu.

Hayo yalisemwa na Mtakwimu Mwandamizi kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Salma Seleh Ali alisema wakati akitoa taarifa ya mfumko wa bei kwa kipindi cha Septemba.

Alisema hali hiyo ya mfumko wa bei imechangiwa kwa kuongezeka bei za vyakula na vivywaji visivyo na vileo kwa asilimia 13.44 kwa mwezi wa Septemba ikilinganishwa na asilimia 11.66 kwa Agosti mwaka huu.

Alisema bidhaa zilizochangia kuongezeka kwa mfumko huo ni mchele wa mapembe asilimia 37.58, mchele wa Mbeya 15.13, unga wa ngano asilimia 3.88 na unga wa sembe asilimia 11.02. Bidhaa zingine ni sukari nyekundu asilimia 29.87, sukari nyeupe asilimia 27.37 na mafuta ya dizeli asilimia 0.74.

Watalamu wa uchumi wanasema kuwa kupanda kwa mfumko wa bei za bidhaa ikiwemo nishati ya mafuta kunatokana na matatizo mbalimbali duniani ikiwemo vita vya Ukraine na Urusi.

Dk. Estellah Ngoma Hassan kutoka Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), alisema kupanda kwa bei ya mafuta kunasababisha bidhaa nyingi kupanda bei na kuathirika kiuchumi.

Mchumi Mandamizi kutoka Benki Kuu ya Tanzania, Ofisi ya Zanzibar, Dk. Uurick Mumbali, alisema chakula kinachotumika Zanzibar asilimia kubwa ni cha kuagiza nje ya nchi, hivyo matatizo yanayotokea duniani ikiwemo vita huleta athari.

Alisema, matatizo yanayotokea duniani kuhusu kupanda kwa bei ya mafuta linaathiri nchi zote hata zile ambazo hazizalishi mafuta.

Rahma Suleiman kutoka Tume ya Ushindani wa Chakula Zanzibar, akizungumzia kuhusu mfumko wa bei ya sukari, alisema hivi karibu mfumuko huo unatarajiwa kupungua kwa sababu kiwanda cha sukari Zanzibar kimeanza uzalishaji.




Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo TIB, Robert Ndaki (katikati), akikata keki na baadhi ya wateja na wafanyakazi wa benki hiyo kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja 2023 katika hafla fupi iliyofanyika jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Majaji, mahakimu wakumbushwa kuongeza ufanisi kazini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAJAJI na mahakimu wametakiwa kuongeza ufanisi wa kazi, kuhakikisha kwamba changamoto zinazowakabili wananchi ikiwemo kusikiliza kesi kwa wakati na kutoa hukumu ikiwa ni sehemu ya kutekeleza dhana ya utawala bora na sheria.

Hayo yalisemwa na Jaji Mkuu wa Zanzibar, Khamis Ramadhan Abdalla katika hafla ya kuamuaga Jaji Abdulhakim Ameir Issa ambaye hivi karibuni ameteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Rufaa Tanzania, uteuzi ambao umefanywa na Rais Dk.Samia Suluhu Hassan.

Alisema, kasi ya hukumu zinazotolewa kwa wananchi ndiyo majukumu ya muhimili wa Mahakama Kuu nchini, hatua ambayo ni sehemu ya utekelezaji wa utawala bora.

Alisema maboresho makubwa yaliyofanywa na Mahakama Kuu katika kipindi cha miaka miwili na nusu sasa matunda yake yanaonekana ikiwemo kuongeza idadi ya mahakimu wa mahakama za mwanzo pamoja na kesi za udhalilishaji wa kijinsia.

Aliwataka mahakimu na majaji kuiga mfano wa Jaji Issa ambaye utendaji wake wa kazi na uwajibikaji ndiyo kigezo cha kumfanya kupanda ngazi na kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Rufaa nchini.

"Majaji na mahakimu wengine tunapaswa kuiga mfano wa Jaji Issa katika utendaji wake wa kazi na majukumu yake ambapo leo hii tunashuhudia kupanda ngazi na kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Rufaa nchini"alisema.

Akizungumza katika hafla hiyo, Jaji wa Mahakama Kuu ya Rufaa Abdulhakim Ameir Issa aliwataka wafanyakazi wenzake katika muhimili wa tatu wa dola Mahakama kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao vizuri na kutoa haki pale panapostahiki kwa mujibu wa sheria.

Alisema wananchi wanahitaji kuona ufanisi wa usikilizaji wa mashauri yao kwa wakati na kutolewa maamuzi ambao ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu kwa mujibu wa sheria.

Aliyataja baadhi ya mafanikio yake katika utendaji wa kazi ni pamoja na nidhamu na Ushirikiano pamoja na kujiendeleza katika elimu kwa sababu kila siku yapo mabadiliko mengi yanayofanyika ikiwemo katika sheria za mwenendo wa makosa ya jinai.

Naye Kadhi mkuu wa Zanzibar, Sheikh Hassan Othman Ngwali aliwataka watendaji katika mhimili wa Mahakama kufanya kazi kwa kuiga utendaji wa uwajibikaji katika utumishi wa serikali na kusikiliza mashauri ya wananchi kwa wakati.

Alisema kitendo cha kuchelewesha kusikiliza mashauri na kuyatolea maamuzi husababisha malalamiko yanayotokana na maumivu kwa jamii na kuona Mahakama ni kama sehemu ya adhabu kwao na sio kimbilio la kusikiliza kesi zao.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**FOMU MADAI – No. 3**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MAGU**
**Kituo cha NYANGUGE Mkoa wa MWANZA**
**Shauri la Madai Na. 14/2023.**
**JINA LA MDAI: VICENT KATALE**
**JINA LA MDAIWA: SHIJA STEPHANO ABEL**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu za mashauri ya madai katika Mahakama za Mwanzo)**

Kwa: SHIJA STEPHANO ABEL WA MTAA MAJENGO – NYANGUGE
Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba
**MADAI YA THS. 540,000/- (LAKI TANO NA ELFU AROBAINI TU).**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 13 Mwezi wa 10 Mwaka 2023 saa 2:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wew kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na kupigwa Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 06 Mwezi wa 10 Mwaka 2023.

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**FEDRICK ANDREA NYALUKE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI YENYE USAJILI **MC 571 BVF** YENYE RANDI YA BLUE , ENGINE NO **AZZWHM34310.** YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAWE. POLISI TAARIFA **IRI/IRI/RB/111708/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**HATI YA KIAPO**

MIMI MIKIDADI JUMA MUZO KABILA MHAYA DINI MUISLAMU KAZI MSTAAFU MKAZI WA MBWENI – DAR ES SALAAM. Nikiwa na akili zangu timamu naapa na kuthibitisha kwamba:

- Kwamba, Mimi MIKIDADI JUMA MUZO, mnamo tarehe 26/9/2023 nilipotelewa na OFA YA KIWANJA, KIWANJA NAMBA 62 KITALU N KISEKE, MWANZA MANISPAA.
- Kwamba, OFA YA KIWANJA hicho tajwa hapo juu kilisomeka kwa majina ya MIKIDADI JUMA MUZO pamoja na jitihada za kukitafuta OFA YA KIWANJA tajwa hapo juu sikufanikiwa kuipata.
- Kwamba, hivyo nimetoa taarifa katika kituo cha Polisi Msimbazi na kupewa LOSS REPORT yenye RB PHQ/KAT/MPI/526/2023.

Nathibitisha kuwa hayo niliyotamka hapo juu ni kweli. Endapo itagundulika kinyume na kiapo hiki hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yangu.
Kwa kuwa mtoa kiapo ni mtu mzima mwenye akili timamu nakubali kiapo chake.
Sahihi ya mtoa kiapo
Kiapo hiki kimetolewa mbele yangu na kupigiwa chapa ya muhuri wa kamishina wa viapo leo hii tarehe 27/9/2023

MBELE YANGU:
JINA: TEDDY M. CHARLES
CHEO: KAMISHNA WA VIAPO
SAHIHI: ..................
TAREHE: 27/9/2023

## KUPOTELEWA NA CHETI



**KENANI ELIEZA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne kilichotolewa na ARUSHA SEKONDARI mwaka 1983. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/23377/2023.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 113 OF 2022**

**In the matter of the estate of the late WITO WILIAM CHIMANGA of ILAZO within Dodoma Region**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**

**BY FESTO WILIAM CHIMANGA**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN. 369 OF 163)**

**ALL PERSONS** Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Admirations made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 10 Day of 10, 2023.

**Presented for filing this 4 day of 9, 2023**

RESIDENT MAGISTRATE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na. 68/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU JUMA ALLY MBUVA wa Chinangali West**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA ALLY JUMA MBUVA**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 23 Mwezi 10 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe ....... Mwezi 10 Mwaka 2023.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KAGEMBE** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye jina la umiliki **MOHAMED ENTERPRISES LTD** yenye usajili namba **MC 956 CVD**, CHASSIS NAMBA: **MD2B15BX7MWK90697** na ENGINE NAMBA: **NOJVXWMK19018.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **PHQ/ARU/ARU/3989/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



RAMADHAN ATHUMANI KASIMU anatangaza kupotea kwa chati cha kidato cha nne chenye index namba S0792/0081/2020 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia MANGAKA DAY SECONDARY SCHOOL mwaka 2020. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: MTW/MAS/RB/224216/2023

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0677020701**
**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**
**WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Watanzania 2 hawajulikani waliko Israel

**TEL AVIV,** Israel

UBALOZI wa Tanzania nchini Israel unasema kuwa hauna mawasiliano na raia wake wawili ambao wanakaa eneo la kusini ambalo limeshuhudia mapambano baina ya wanamgambo wa Kipalestina wa Hamas na Jeshi la Israeli.

Akizungumza na BBC, Balozi wa Tanzania nchini Israel, Alex Kallua, alisema mpaka jana asubuhi, ubalozi huo umekuwa na mawasiliano na Watanzania takribani 350 waliopo nchini humo kasoro wanafunzi hao wawili.

"Tunaendelea kuwafuatilia Watanzania wawili ambao ni wanafunzi waliokuwa wanafanya mafunzo kwa vitendo 'internship' kusini mwa nchi hiyo. Tunafanya jitihada za kuwapata kwanza ili kufahamu walipo na hali zao.

"...wanafunzi wengine takribani 260 kati ya Watanzania zaidi ya 350 wako salama katika maeneo mbalimbali nchini humo na wamekuwa na mawasiliano na ubalozi," alisema.

Balozi huyo aliongeza kuwa wanaendelea kufuatilia hali ya usalama nchini humo ili kuhakikisha kila Mtanzania anakuwa salama.

**Tunafuatilia kwa karibu, na tunaendelea kupata taarifa kutoka Mamlaka za Israel kuhusu hali ilivyo, tunaendelea kufuatilia na kuwaeleza waliopo na hali ilivyo**

"Tunafuatilia kwa karibu, na tunaendelea kupata taarifa kutoka Mamlaka za Israel kuhusu hali ilivyo, tunaendelea kufuatilia na kuwaeleza waliopo na hali ilivyo," alisema.

Inaelezwa kuwa mapambano kati ya Israel na wapiganaji wa Hamas yameendelea hadi jana katika miji ya kusini mwa Israel. Na kwamba idadi ya vifo na majeruhi inazidi kuongezeka huku maelfu ya watu wakilazimika pia kuyahama makazi yao.

Msemaji wa Jeshi la Israel, Richard Hecht, amesema bado wanapambana katika angalau maeneo saba yaliyopo kusini karibu na eneo la pwani, lakini taarifa ya jeshi hilo inasema wamechukua udhibiti wa maeneo yaliyoshambuliwa na Hamas.

Ilielezwa kuwa serikali ya Tel Aviv iliwatuma maelfu ya wanajeshi katika Ukanda wa Gaza na imeapa kulishinda kundi hilo la wanamgambo wa Kipalestina.

Jeshi la Israel lilianzisha mashambulizi makubwa ya anga baada ya kundi la Hamas kuivamia Israel kwa kushtukiza Jumamosi kwa kurusha maelfu ya makombora huku mamia ya wapiganaji wakiingia hadi Israel na kufanya mauaji.

Israel ilieleza kuwa imeshtushwa na shambulio hilo ambalo halijawahi kushuhudiwa katika eneo lake na kwamba hadi sasa zaidi ya watu 700 wameuawa Israel huku 430 wakiuliwa huko Gaza. Ilibainishwa kuwa mwishoni mwa juma, Hamas waliwaua takriban watu 250 waliokuwa wakihudhuria tamasha la muziki karibu na Gaza.

### HATUA ZA ISRAEL

Waziri wa Ulinzi wa Israel, Yoav Galant, aliamuru kuzingirwa kwa Gaza, akisema mamlaka itakata umeme na kuzuia kuingia kwa chakula na mafuta eneo hilo. Huku ikiwaita takriban askari wa akiba 300,000 ili kujibu mashambulizi makubwa ya wanamgambo wa Hamas.

Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, aliwaonya raia wa Gaza kuondoka katika maeneo yote ya Hamas ambayo ameapa kuyasambaratisha na kuyageuza kuwa vifusi.

Wapalestina katika eneo la pwani lenye watu milioni 2.3 wamejiandaa kwa kile ambacho wengi walihofia kuwa litakuwa shambulio kubwa la ardhini la Israel linalolenga kuwashinda wanamgambo wa Hamas na kujaribu kuwakomboa mateka wasiopungua 100.

### MAELFU WAHAMA

Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Uratibu wa Masuala ya Kibinadamu (OCHA) ilisema zaidi ya Wapalestina 123,000 katika Ukanda wa Gaza wamekuwa wakimbizi wa ndani kutokana na mashambulizi ya kulipiza kisasi ya Israel katika ukanda huo.

Shirika hilo lilisema watu wamelazimika kukimbia kwa kuhofia usalama wao au kutokana na nyumba kuharibiwa.

Wizara ya masuala ya Umma na Makazi ya mjini Gaza ilisema nyumba 1,210 zimeharibiwa vibaya kutokana na mashambulizi ya anga ya Israel, ambayo pia yamesababisha uharibifu wa vituo vya afya na miundombinu ya usambazaji wa majisafi na kuwaathiri zaidi ya watu 400,000.

Marekani imeahidi kuiunga mkono Israel ambayo ni mshirika wake mkuu na kusema kuwa itatuma silaha na vifaa vya kijeshi. **BBC/DW**



Wananchi wawili wa Palestina wakishuhudia nyumba zilizoharibiwa na mashambulizi ya Israel huko Rafah kusini mwa Gaza. **PICHA: MTANDAO**

# Shule zafungwa kutokana na kunguni

**PARIS,** Ufaransa

WAZIRI wa Elimu wa Ufaransa, Gabriel Attal, amesema kuwa nchi hiyo imelazimika kufunga shule saba zinazowapokea wanafunzi 1,500 baada ya kuvamiwa na kunguni.

Siku chache zilizopita, mamlaka ya Paris ilitangaza kufungwa kwa shule mbili kwa sababu ya kunguni, moja ikiwa Marseille na nyingine Villefranche-sur-Saone nje kidogo ya mji wa kusini mashariki mwa Lyon.

Ilielezwa kuwa serikali ya Ufaransa imefanya msururu wa mikutano siku chache zilizopita kuchunguza idadi inayoongezeka ya visa vya kunguni, wakati nchi hiyo ikiandaa Kombe la Dunia la Rugby na ambayo itakuwa mwenyeji wa Michezo ya Olimpiki 2024.

Pia ilielezwa kuwa serikali imelazimika kuingilia kati kupambana na kunguni hao. Huku Waziri Mkuu wa Ufaransa Elisabeth Borne, akiitisha kikao cha baraza la mawaziri kujadili namna ya kupambana na kunguni hao.

Waziri wa Usafiri, Clement Beaune, alikutana na kampuni za usafirishaji kubuni mpango wa kufuatilia na kunyunyizia dawa vyombo vya usafiri wa umma, kujaribu kupunguza wasiwasi nchini humo.

Baada ya taarifa kuwa kunguni walipatikana kwenye jengo la sinema mwezi mmoja uliopita, raia wa Ufaransa walianza kusambaza video katika mitandao ya kijamii zikionesha wadudu hao wakitambaa majumbani na kwenye usafiri wa umma kama matreni na mabasi.

Kunguni wamekuwapo Ufaransa na mataifa mengine ya Ulaya kwa miongo kadhaa na hakuna mwenye kinga ya kuvamiwa na wadudu hao. Huku mtaalamu wa wadudu kwenye Hospitali ya Chuo Kikuu cha Mediterenia mjini Marseille, Ufaransa, Jean-Michel Berenger, alisisitiza kuwa kunguni hawatokani na uchafu, bali wanachofuata ni damu ya mtu.

Meya wa Jiji la Amiens, Brigitte Foure, alisema maktaba moja ya manispaa inatarajiwa kufunguliwa tena baada ya kufungwa kwa siku kadhaa baada ya kunguni kugunduliwa katika maeneo ya kusomea vitabu, akisisitiza kuwa mbwa wa kunusa hawakugundua uwepo wowote wa wadudu hao baada ya maktaba hiyo kushughulikiwa.

Takwimu za Shirika la Afya na Usalama wa Chakula nchini Ufaransa zinaonyesha kuwa angalau nyumba moja kati ya kumi nchini humo ilikuwa na kunguni katika miaka michache iliyopita.



Kunguni wameripotiwa sehemu mbalimbali nchini Ufaransa kama kwenye treni za mwendo kasi katika mji mkuu Paris, na hata katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Charles De Gaulle. **DW**

# CHABRUMA ATAKA ZAIDI KWA TANZANITE KOMBE LA DUNIA

**Na Saada Akida**

LICHA ya ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya Djibouti, Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Wasichana chini ya miaka 20 (U-20) ,'Tanzanite', Esther Chabruma, amesema timu yake bado ina mapungufu kadhaa, hivyo anarudi kwenye uwanja wa mazoezi kuyafanyia kazi yote yaliyojitokeza kwenye mchezo uliopita.

Tanzanite iliibuka na ushindi huo katika mchezo ya kwanza dhidi ya Djibouti kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia, uliopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam na timu hizo zikitarajia kurudiana tena kesho katika dimba hilo.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Chabruma, alisema wanaenda kufanya maboresho na mapungufu yaliyojitokeza kwenye mchezo wa juzi ikiwa ni maandalizi ya mechi ya marudiano.

**Alisema walicheza nao mechi ya kwanza na kushinda mabao 5-0 lakini ameona mapungufu ya kikosi chake yanayohitaji kufanyiwa kazi kwa ajili ya kupambana kesho.**

"Tumefanya vizuri katika mchezo huu na kupata ushindi, lakini hatuwezi kusema tumefuzu moja kwa moja kwa sababu kuna mechi ya marudiano tunakutana nayo tena Djibouti hatuwezi kujua wenzetu wanakuja kwa staili gani.

"Tunaenda kujiandaa vizuri kufanyia kazi mapungufu yetu, lakini pia ubora wa Djibouti ili kutafuta ushindi kwenye mechi yetu ya marudiano na kufuzu kucheza Kombe la Dunia," alisema Chabruma.

Aliongeza kuwa wana siku mbili za kujiandaa kwa mchezo huo na anaimani watazitumia vizuri kwa ajili ya kufanyia kazi mapungufu yao.




Kiungo Mshambuliaji wa Simba, Clatous Chama, akiachia shuti huku akizingirwa na wachezaji wa Singida Fountain Gate FC, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Liti juzi na Simba kuibuka na ushindi wa mabao 2-1. **PICHA: SIMBA**

# *Mtibwa yamfungua mdomo Minziro*

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kuonja ushindi wa kwanza kwenye Ligi Kuu Bara msimu huu, Kocha Mkuu wa timu ya Tanzania Prisons, Fred Felix Minziro, amesema ndio kwanza wameanza ligi hiyo na moto utaendelea kuwaka.

Prisons juzi ilifanikiwa kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Turiani mkoani Morogoro, huo ukiwa ni ushindi wao wa kwanza msimu huu baada ya mechi tano.

Matokeo hayo yanaifanya Prisons sasa kufikisha pointi nne katika nafasi ya 13, kutokana na kutoka sare mechi moja na kupoteza tatu. Akizungumza na gazeti hili jana, Minziro alisema amefurahishwa na kiwango kilichooneshwa na wachezaji wake na kudai moto umeanza kuwaka.

"Nimefurahi kuona timu yangu leo imeweza kupata ushindi ikiwa ni mara yetu ya kwanza tangu msimu huu ulipoanza," alisema Minziro.

Kocha huyo aliongeza kuwa mchezo huo ulikuwa na ushindani mkubwa kwani mpinzani wake aliingia uwanjani akiwa na matumaini ya kupata pointi tatu, lakini hali haikuwa hivyo na kujikuta akiangukia kipigo.

Alisema licha ya ushindi huo yapo makosa madogomadogo ambayo ameyabaini na kuahidi kurudi katika uwanja wa mazoezi kuyafanyia kazi kwa ajili ya kujiandaa na michezo ijayo.

Kwa upande wa Mtibwa Sugar kipigo hicho kinaifanya kushika nafasi ya pili kutoka mkiani kwenye msimamo wa ligi hiyo inayojumuisha timu 16, hiyo ni kutokana na kukusanya alama mbili tu katika michezo mitano hadi sasa.

Simba ndiyo kinara wa ligi hiyo, ikiwa na alama 15, kutokana na ushindi asilimia 100 iliyoupata, huku Azam FC ikifuata kwa pointi 13, kisha Yanga yenye alama 12 na KMC FC ikifunga kazi kwenye nne bora ikiwa na pointi 10, timu zote zikiwa zimecheza mechi tano kila moja.

## Zimamoto yatoa sababu vichapo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa Zimamoto, Mohmed Hilali 'Tedy', amesema kuwapo kwa majeruhi wengi katika kikosi chake cha kwanza ndiko kunakoitesa timu hiyo na kusababisha kufanya vibaya katika michezo mitatu mfululizo.

Zimamoto juzi ilikubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya wanajeshi wa Kipanga katika mchezo wa kukamilisha mzunguko wa tano wa Ligi Kuu Zanzibar inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar, PBZ.

Akizungumza na Nipashe juzi, kocha huyo alisema kupoteza michezo mitatu mfululizo kumetokana na kuwakosa wachezaji wake tegemeo ndani ya kikosi hicho ambao ni majeruhi.

Alisema hali hiyo inampa wakati mgumu wa kupanga kikosi ambacho kitapata matokeo mazuri kutokana na wachezaji anaolazimika kuwatumia kwa sasa bado hawajawa na uzoefu mkubwa kwenye Ligi Kuu.

Alisema kuelekea mechi yao ya raundi ya sita, mpaka sasa bado hajapata uhakika wa kuwatumia wachezaji wake wanne kutoka chumba cha madaktari.

"Ligi yetu kama inavyoonekana hivi sasa inakasi kubwa, kila timu inataka kupata alama za mapema, nimejaribu kuwapandisha wachezaji wawili kutoka timu ndogo, lakini tulichofanikiwa ni kupunguza idadi ya magoli ya kufungwa, nafikiri bado wachezaji hawa hawajazoea mikikimikiki ya Ligi Kuu, hiyo ikiwa ndio mechi ya pili kwao kucheza," alisema Kocha Tedy, ambaye kikosi chake kitashuka tena dimbani Jumapili wiki hii dhidi ya Mlandege FC.

## Makocha kuogelea wanolewa siku 3

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kupigwa darasa la siku tatu kuongeza ujuzi, makocha wa timu za kuogelea, wametakiwa kuyafanyia kazi kwa vitendo mafunzo waliyopata ili kwenda kuibua na kukuza vipaji vya wachezaji wa mchezo huo katika maeneo ya kazi.

Akizungumza na gazeti hili jana, wakati wa kufunga mafunzo hayo ya siku tatu ya makocha wa kuogelea yaliyokuwa yakifanyika jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Ufundi wa Chama cha Kuogelea Tanzania (TSA) Amina Mfaume, aliwataka makocha hao kwenda kuyafanyia kazi yote waliyofundishwa ili waweze kuufikisha mbali mchezo huu.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuona wachezaji wanazidi kubadilika na kuukuza mchezo wa kuogelea hapa nchini.

HABARI MICHEZO

ZISIKUPITE

### GIROUD KIPA MILAN

AC Milan wamemuongeza mshambuliaji wa Ufaransa, Olivier Giroud, kwenye orodha rasmi ya makipa wa kikosi chao baada ya kuokoa muda wake wa kusimama langoni katika mechi ya Jumamosi dhidi ya Genoa. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37, alichukua glovu kutokana na kadi nyekundu ya dakika ya 97 kwa kipa Mike Maignan. ***(442)***

### TATA HAJUI KUHUSU MESSI

KOCHA Mkuu wa Inter Miami, Tata Martino, amesema "sijui lolote" kuhusu uvumi unaomhusisha gwiji wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 36, na kuhamia Barcelona kwa mkopo wakati wa mwisho wa msimu wa Ligi Kuu ya Marekani, utakaoanza mwishoni mwa Oktoba hadi Februari mwakani. ***(Goal)***

### ROONEY KOCHA BIRMINGHAM

WAYNE Rooney mwenye umri wa miaka 37, yuko mbioni kuwa kocha wa Klabu ya Birmingham City baada ya kuacha nafasi yake kama kocha mkuu wa DC United inayoshiriki Ligi ya Marekani, MLS. (Times)

### STEIJN KUJADILIWA AJAX

AJAX itajadili mustakabali wa Kocha Mkuu, Maurice Steijn, baada ya timu hiyo ya Uholanzi kushuka katika timu tatu za mkiani kutokana na kufungwa mechi tatu mfululizo kwenye Ligi Kuu Uholanzi, Eredivisie. ***(Fabrizio Romano)***

### VAN GAAL ASHUHUDIA

ALIYEKUWA Kocha wa Ajax, Louis van Gaal, ambaye hivi majuzi alijiunga na bodi ya usimamizi ya klabu hiyo, alikuwa kwenye viti kutazama kichapo chao cha hivi karibuni cha mabao 2-1 nyumbani dhidi ya AZ Alkmaar juzi, Jumapili. (***Sport***)

### LORRAN AWANIWA UNITED

KLABU ya Manchester United inawafuatilia kiungo wa Palmeiras, Luis Guilherme na winga wa Flamengo, Lorran, kila mmoja akiwa na umri wa miaka 17, lakini wanaweza kulazimika kutumia hadi pauni milioni 100 kuwapata vijana hao wa Brazil. ***(Star)***

### SEVILLA NA KOCHA MPYA

KLABU ya Sevilla inatarajia kupata mbadala wa haraka baada ya juzi, Jumapili kumtimua Jose Luis Mendilibar. Kocha huyo aliisaidia Sevilla kushinda taji la saba la Ligi ya Europa msimu uliopita, lakini ameiongoza kushinda mara mbili pekee kati ya mechi nane katika kampeni za sasa za LaLiga. ***(AS)***

### AWANIWA BRENTFORD

KLABU ya Brentford inafikiria kumnunua winga wa Sunderland, Jack Clarke kwa pauni milioni 15 Januari. ***(Alan Nixon via Chronicle)***

### ROHL KOCHA SHEFFIELD

DANNY Rohl, 34, ambaye amekuwa na majukumu ya ukocha na RB Leipzig, Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Ujerumani, ameibuka kuwa kocha anayefuata wa Sheffield Wednesday. ***(Mail)***

### REMY ATUNDIKA DALUGA

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Chelsea, Newcastle na Crystal Palace, Loic Remy, 36, ametangaza kustaafu. Mfaransa huyo amekuwa mchezaji huru tangu aachiwe na Brest msimu wa majira ya joto. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA ATHIBITISHA KIKOSI ENGLAND KUMKOSA SAKA

**Hatafanikiwa, hajafanya mazoezi hata mchezo mmoja, hatapatikana kwa sasa...**

**LONDON,** England

BUKAYO Saka hatajiunga na kikosi cha England kwa majukumu ya kimataifa, kwa mujibu wa kocha wa Arsenal, Mikel Arteta.

**Saka alikosekana katika ushindi wa bao 1-0 wa 'Washikabunduki' hao dhidi ya Manchester City Jumapili kutokana na kusumbuliwa na tatizo la misuli ya paja katika mechi za hivi karibuni.**

Kukosekana kwa Saka kulimaliza msururu wake wa kucheza mechi 87 mfululizo za Ligi Kuu na Arteta alisema sasa hatashiriki mechi zijazo za England dhidi ya Australia Ijumaa na Italia Oktoba 17.

Arteta alisema: "Hapana, hatafanikiwa. Hajafanya mazoezi hata mchezo mmoja. Hatapatikana kucheza soka kwa sasa."

Winga huyo mwenye umri wa miaka 22, alichechemea wakati Arsenal ilipopoteza dhidi ya Lens Jumanne iliyopita, baada ya kutolewa pia katika ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Bournemouth.

Kocha wa England, Gareth Southgate, Alhamisi alisema kwamba hatajiweka hatarini na Saka licha ya mechi dhidi ya Italia itakuwa muhimu ya kufuzu kwa michuano ya Euro.

Southgate alisema mapema: "Naweza tu kupitia kile Mikel (Arteta) amesema kuhusu mechi chache zilizopita.

"Tunawaangalia wachezaji kama vile nchi yoyote. Siku zote kuna umakini kwa wachezaji wetu kwa sababu wanacheza mpira na klabu zao.

"Wakati mataifa mengine yote yanawaita wachezaji wanaocheza Ligi Kuu na hakuna anayeangalia jinsi wanavyowatunza na jinsi wanavyowafundisha.

"Tunapokuwa na mazungumzo mazuri na klabu zote, nadhani wote watakubali kwamba labda tutatoa maoni bora kuliko kila taifa lingine.

"Wana imani na sisi kwamba tunafanya maamuzi ambayo ni sahihi kwa muda mrefu wakati wowote tunapoweza. Tuna mechi 10 tu kwa mwaka. Na kuna wakati Bukayo, kwa mfano, hatujacheza kila wakati.

"Lakini kuna michezo fulani muhimu ambapo ikiwa inawezekana kuwa kwa wachezaji wako bora, basi unataka kuwa nao.

"Kwa hiyo tuna jukumu hilo la kufuzu kwa nchi lakini - nimekuwa mchezaji - sijawahi kuhatarisha afya ya mwili ya mchezaji. Na mimi pia."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 738,

MECHI KALI
PORTSMOUTH
VERSUS
GILLINGHAM
1 | 1.52
X | 3.97
2 | 5.29

tigo pesa SportPesa
WASHINDI WA MAOKOTO Deilee!
1. Ally Dume - 0652 292 XXX
2. Paul John - 0658 453 XXX
3. Mbarouk Mbarouk - 0659 493 XXX
4. Dubwana Omary - 0673 290 XXX
5. Kombo Swalehe - 0673 555 XXX
6. Akreyson Kizibwe - 0679 613 XXX
7. Musa Bukwimba - 0679 749 XXX
8. Hendrick Nyoni - 0712 447 XXX
9. Innocent Mitwango - 0714 800 XXX
10. Jackson Godfrey - 0716 968 XXX
20,000/= KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588 0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MESSI KURUDI BARCA JANUARI



**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi anaweza kujiunga tena na Barcelona kwa mkopo kutoka Inter Miami baada ya kushindwa kufuzu kwa mechi za mchujo za Ligi Kuu ya Marekani (MLS), ripoti zimeeleza.

Kipigo cha Miami cha bao 1-0 kutoka kwa Cincinatti, kilithibitisha kwamba hawatashiriki katika hatua inayofuata ya mashindano hayo, na msimu wao utamalizika baadaye mwezi huu.

Msimu wake wa kwanza nchini Marekani, Messi amefikisha mabao 11 katika michezo 13, ingawa alifanya vema zaidi kwenye Kombe la Ligi ikilinganishwa na mashindano mengine.

Msimu wa kutatanisha wa Miami unaweza kufungua uhamisho wa mkopo kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36, huku ripoti za Sport zikidai watakuwa tayari kumruhusu ajiunge na Barcelona Januari.

Messi alijijengea heshima yake kama mmoja wa wanasoka bora wa muda wote pale Nou Camp, akishinda mataji tisa ya ligi, saba ya Copa del Reys, manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na tuzo saba za Ballon d'Or.

Pia, aliifungia Barca mabao 673, huku mabao 72 akifunga msimu wa 2011-12 pekee.

Barca walikuwa na nia ya kumsajili kabla ya kuhamia Marekani, lakini wameona biashara yao ya uhamisho ikitatizwa katika miaka ya hivi karibuni na matatizo ya kifedha.

Messi hatakuwa mchezaji wa kwanza wa MLS kurejea Ulaya kwa mkopo ikiwa atakamilisha uhamisho huo.



## 'FIFA imekosea Kombe la Dunia nchi 6'

**ZURICH,** Uswisi

RAIS wa zamani wa Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), Sepp Blatter, amekosoa uamuzi wa shirikisho hilo kuandaa kombe la dunia la mwaka 2030 katika mataifa sita na mabara matatu.

Morocco, Hispania na Ureno zilitawazwa kuwa wenyeji wa michuano hiyo ya mwaka 2030, huku Uruguay, Argentina na Paraguay pia zikiwa mwenyeji wa mechi za ufunguzi kuadhimisha miaka 100 ya michuano hiyo, FIFA ilisema katika taarifa yake Jumatano.

Uamuzi huo umekosolewa na Blatter, ambaye alikuwa rais wa FIFA kuanzia mwaka 1998 hadi 2015, kabla ya kulazimika kutolewa baada ya madai ya rushwa.

"Ni upuuzi kusambaratisha mashindano kwa njia hii," alisema Blatter akiliambia gazeti la SonntagsBlick la nchini Uswisi.

"Fainali za Kombe la Dunia lazima ziwe tukio fupi," alisema, akiongeza hii ilikuwa muhimu kwa utambulisho wa hafla hiyo, kwa shirika na kwa wageni.

Blatter, ambaye zamani alikuwa mmoja wa watu mashuhuri katika kandanda, aliwahi kuikosoa FIFA kwa kuipa Qatar mashindano ya 2022, akisema nchi hiyo ya Mashariki ya Kati ni ndogo sana.

Blatter mwenye umri wa miaka 87, alisema mashindano ya mwaka 2030 yanapaswa kufanyika Amerika Kusini, kuadhimisha kumbukumbu ya miaka 100 ya tukio la kwanza ambalo liliandaliwa nchini Uruguay.

,772,220

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 11/10/23 | 23:15 | Bogota vs Cortulua | 2.14 | 3.01 | 3.32 |
| 2. 11/10/23 | 23:15 | Real Soacha vs Real Santander | 2.39 | 3.01 | 2.86 |
| 3. 12/10/23 | 02:15 | Deportivo Cali vs Deportes Tolima | 2.33 | 2.96 | 3.01 |
| 4. 12/10/23 | 04:05 | Tapatio vs Leones Negros | 2.15 | 3.26 | 3.05 |
| 5. 12/10/23 | 17:00 | Azerbaijan U21 vs Northern Ireland U21 | 2.79 | 3.20 | 2.33 |
| 6. 12/10/23 | 19:00 | Russia vs Cameroon | 2.27 | 3.23 | 3.23 |
| 7. 12/10/23 | 19:00 | Slovakia U21 vs Poland U21 | 2.37 | 3.20 | 2.74 |
| 8. 12/10/23 | 21:45 | Albania vs Czech Republic | 3.22 | 3.17 | 2.30 |
| 9. 13/10/23 | 17:00 | Greece U21 vs Croatia U21 | 2.70 | 3.05 | 2.36 |
| 10. 13/10/23 | 19:00 | Estonia vs Azerbaijan | 2.21 | 3.12 | 3.49 |
| 11. 13/10/23 | 21:45 | Austria vs Belgium | 2.70 | 3.28 | 2.60 |
| 12. 13/10/23 | 21:45 | Ireland vs Greece | 2.43 | 3.11 | 3.06 |
| 13. 13/10/23 | 22:00 | Real Oviedo vs Albacete | 2.31 | 2.88 | 3.23 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 10/10/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 4779 | Kirsehir Belediye Spor vs Sirnak Idmanyurdu | 1.69 | 3.72 | 4.18 |
| 14:30 | 1929 | Guangxi Pingguo Haliao F.C. vs Sichuan Jiuniu | 4.38 | 3.06 | 1.84 |
| 14:30 | 4504 | Hebei Kungfu vs Jiangxi Liansheng | 1.33 | 4.49 | 8.16 |
| 14:35 | 4475 | China vs Vietnam | 1.52 | 4.07 | 6.34 |
| 16:05 | 4756 | Bahla vs Sohar Club | 3.40 | 3.15 | 2.05 |
| 16:20 | 4723 | Dhofar Salalah vs Ibri | 1.62 | 3.41 | 5.29 |
| 17:00 | 2999 | Isparta 32 Spor vs Sincan Belediyespor | 1.47 | 4.38 | 5.29 |
| 17:00 | 3683 | Buqaa Amman vs Alia Club | 1.72 | 3.37 | 4.49 |
| 19:00 | 2210 | LYS Sassandra vs Racing Club Dabidjan | 2.80 | 3.05 | 2.41 |
| 19:30 | 3814 | FB Brindisi vs Juve Stabia | 2.34 | 3.14 | 3.08 |
| 20:00 | 2695 | SV Heimstetten vs TSV Dachau | 1.52 | 4.17 | 4.99 |
| 20:00 | 4993 | SC Eltersdorf vs ASV Neumarkt | 1.42 | 4.50 | 5.20 |
| 20:00 | 5274 | Bursaspor vs Golcukspor | 1.56 | 3.95 | 4.40 |
| 21:00 | 1204 | Mansfield vs Doncaster | 1.55 | 3.93 | 5.00 |
| 21:00 | 1816 | Claypole vs Ferrocarril Midland | 2.22 | 2.91 | 3.27 |
| 21:00 | 1936 | Reading vs Swindon Town | 1.82 | 3.76 | 3.51 |
| 21:00 | 2076 | Stevenage vs Wycombe | 1.93 | 3.36 | 3.51 |
| 21:00 | 2107 | Walsall vs Forest Green | 2.05 | 3.40 | 3.15 |
| 21:00 | 2194 | Csyd Liniers vs Deportivo Laferrere | 2.80 | 2.80 | 2.59 |
| 21:00 | 2295 | Central Cordoba vs Excursionistas | 3.25 | 2.90 | 2.14 |
| 21:00 | 2461 | Lujan vs Leandro N Alem | 1.57 | 3.47 | 5.71 |
| 21:00 | 2918 | Tranmere vs Leicester U21 | 1.63 | 4.07 | 4.17 |
| 21:00 | 2943 | Carlisle vs Nottingham U21 | 1.51 | 4.19 | 5.01 |
| 21:00 | 2987 | Notts County vs Derby | 2.90 | 3.62 | 2.09 |
| 21:00 | 3126 | Blackpool vs Liverpool U21 | 1.39 | 4.58 | 6.10 |
| 21:00 | 3228 | Berazategui vs CA Atlas | 2.06 | 3.11 | 3.42 |
| 21:00 | 3668 | Sportivo Italiano vs Yupanqui | 1.40 | 4.27 | 6.51 |
| 21:00 | 3961 | Lincoln vs Wolverhampton U21 | 1.53 | 4.17 | 4.88 |
| 21:00 | 4206 | Charlton vs Aston Villa U21 | 1.52 | 4.17 | 4.99 |
| 21:00 | 4481 | Morecambe vs Barrow | 2.60 | 3.22 | 2.47 |
| 21:00 | 4733 | Satsaid W vs CA River Plate W | 4.90 | 3.60 | 1.57 |
| 21:00 | 5496 | Deportivo Espanol vs Puerto Nuevo | 1.78 | 3.20 | 4.46 |
| 21:00 | 5747 | Wigan vs Fleetwood Town | 2.14 | 3.40 | 2.95 |
| 21:15 | 5068 | Exeter vs Arsenal U21 | 3.05 | 3.71 | 1.99 |
| 21:30 | 1296 | Crewe vs Wrexham | 3.05 | 3.55 | 2.04 |
| 21:30 | 4058 | Cheltenham vs Newport | 2.17 | 3.40 | 2.89 |
| 21:30 | 4859 | Salford City vs Stockport | 3.05 | 3.41 | 2.09 |
| 21:30 | 5023 | Argentino Rosario vs Deportivo Muniz | 1.69 | 3.15 | 4.70 |
| 21:30 | 5258 | Grimsby vs Bradford City | 2.28 | 3.10 | 2.95 |
| 21:45 | 1115 | Guiseley vs Atherton Collieries | 1.63 | 3.61 | 4.78 |
| 21:45 | 1753 | AFC Hornchurch vs Hastings United | 1.55 | 4.08 | 4.79 |
| 21:45 | 1864 | Galway United vs Waterford Utd | 1.83 | 3.58 | 3.53 |
| 21:45 | 2284 | Radcliffe Borough vs Macclesfield FC | 2.09 | 3.61 | 2.90 |
| 21:45 | 3966 | Billericay Town vs Dulwich Hamlet | 1.83 | 3.67 | 3.57 |
| 21:45 | 4787 | Sutton United vs Crawley Town | 2.20 | 3.32 | 2.91 |
| 21:45 | 4921 | Harrogate vs Accrington | 2.44 | 3.36 | 2.54 |
| 21:45 | 4987 | Whitehawk vs Haringey Borough | 1.76 | 3.71 | 3.81 |
| 21:45 | 5398 | Chesham Utd vs Didcot Town | 1.25 | 5.48 | 8.53 |
| 21:45 | 5406 | Port Vale vs Newcastle U21 | 1.35 | 4.79 | 6.73 |
| 21:45 | 5989 | Portsmouth vs Gillingham | 1.54 | 3.93 | 5.10 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.




# YAO KINARA 'ASSIST' BARA

**Na Saada Akida**

BEKI wa Yanga, Yao Kouassi, raia wa Ivory Coast, anaongoza kwa kutoa pasi za mwisho kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara akiwa amefanya hivyo mara tatu hadi sasa ligi hiyo ikiwa raundi ya tano.

Beki huyo wa kulia aliyesajiliwa msimu huu akitokea Asec Mimosas ya nchini humo, amekuwa mhimili mkubwa kwa Yanga kwenye kusaidia mashambulizi.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa jana na Bodi ya Ligi, Kouassi ana 'assist' tatu, akifuatiwa na nyota wengine wa Yanga, Mudathir Yahaya na Maxi Nzengeli wenye 'assist' mbili kila mmoja.

"Rekodi zetu zinaonesha kuwa 'assist' ya kwanza aliitoa Agosti 23 kwenye Uwanja wa Azam Complex, akimpa Maxi Nzengeli aliyefunga bao la tano, Yanga ikiichapa JKT Tanzania 5-0, ya pili ilikuwa Septemba 20, alipotoa pasi ya mwisho iliyosababisha kufungwa bao pekee dhidi ya Namungo na Mudathir Yahya mechi ikichezwa uwanja huo huo na Jumamosi iliyopita alitoa nyingine kwa Pacome Zouzoua aliyefunga bao la kwanza kwenye mechi ambayo Yanga ilishinda 3-0 dhidi ya Geita Gold, Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza.

Wachezaji wanne wa Simba, Kibu Denis, Luis Miquissone, Mohamed Hussein 'Tshabalala', Shomari Kapombe, nao pia wana 'assist' mbili kila mmoja.

Wengine wenye 'assist' kama hizo ni Awesu Awesu wa KMC, Ladaki Chasambi wa Mtibwa Sugar, Impiri Mbombo wa Tabora United, Cheikh Sidibe wa Azam FC.

Kwa upande wa wafungaji, Jean Baleke wa Simba anaendelea kuwa kinara kwa mabao matano, Feisal Salum wa Azam akifuatiwa na mabao yake manne, lakini baada ya mechi za wiki iliyopita kumekuwa na mchuano mkali juu, kwani tayari Zouzoua, Aziz Ki, Nzengeli wote wa Yanga na Matheo Antony wa Mtibwa, wote wana mabao matatu kibindoni.

## Chama ajitabiria kiatu Ligi Kuu Bara

INATOKA UKURASA 24

Alisema amekuwa akifunga mabao kadhaa kwenye uwanja huo na ana uhakika atafanya hivyo msimu huu, na akiongeza na mabao ambayo kwa sasa anafunga mikoani anaweza kuwa na idadi kubwa ya mabao msimu huu kuliko wakati mwingine wowote.

"Najua Uwanja wa Benjamin Mkapa utafunguliwa muda si mrefu kwa hiyo ni hali nzuri kwangu, naomba Mungu anisaidie na wachezaji wenzangu pia wanipe msaada, naweza kuwa kwenye kinyang'anyiro cha ufungaji bora msimu huu," alisema.

UDHAMINI...




Rais wa Yanga, Injinia Hersi Said (kulia), akimkabidhi jezi Mkurugenzi wa Shirika la Bima la Taifa (NIC), Dk. Elirehema Doriye, baada ya kuingia mkataba wa udhamini wa mchezaji bora wa mwezi wa klabu hiyo kwa kipindi cha miaka mitatu wenye thamani ya Sh. milioni 900. Hafla hiyo fupi ilifanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Ukarabati kwa Mkapa wafikia asilimia 95

**Na Mwandishi Wetu**

UKARABATI wa awamu ya kwanza unaoendelea katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, umefikia asilimia 95 na asilimia tano zilizobaki zinatarajiwa kukamilika ndani ya siku tano kuanzia jana.

Akikagua ukarabati huo jana uwanjani hapo, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, alisema tayari vyumba vinne vya wachezaji vya kubadilishia nguo, sehemu ya kuchezea (pitch), vyumba vya waamuzi, afya na eneo la video za marejeo (VAR) vimekamilika.

"Tayari taa za kisasa 320 za mfumo wa LED zimefungwa na kuna huduma ya mtandao wa bure kabisa wa 'intaneti' kwa ajili ya watazamaji wa mechi ambao tutauzindua kati ya tarehe 17 hadi 19, mwezi huu, kabla ya mchezo wa ufunguzi wa African Football League kati ya Simba na Al Alhy ya Misri Oktoba 20, mwaka huu," alisema Ndumbaro.

Aliongeza kuwa, katika eneo la watu mashuhuri na sehemu ya waandishi wa habari kazi iliyobakia ni ndogo ambayo itamalizika ndani ya siku hizo tano akiongeza kuwa mfumo wa sauti uwanjani tayari umerekebishwa.

Dk. Ndumbaro alisema Kampuni ya Formula 360, itafunga mfumo wa matangazo kidijitali ambao utaanza kufanya kazi rasmi Oktoba 20, mwaka huu, huku akisisitiza kuwa baada ya mchezo huo, ukarabati mkubwa wa awamu ya pili utaendelea.

# Michezo

Jumanne Oktoba 10, 2023

Nipashe




Ukarabati kwa Mkapa wafikia 95%

UKURASA 23

95%...



Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, akikagua nyasi za Uwanja wa Benjamin Mkapa, baada ya kutembelea jana kukagua ukarabati unaoendelea kufanywa. **MPIGAPICHA WETU**

# NYOTA YANGA SASA KUWANIA MAMILIONI

## ●●● NIC yawaongeza ushindani, yawamwagia milioni 900/-, Gamondi naye...

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha ushindani unaongezeka ndani ya kikosi, uongozi wa Klabu ya Yanga, umeanzisha tuzo ya mchezaji bora wa mwezi kama ilivyo kwa watani wao wa jadi, Simba, ambapo kila mwezi humzawadia mshindi shilingi milioni mbili ambayo hutolewa na mdhamini wao, Kampuni ya Emirates.

**Lakini kwa Yanga imeingia udhamini wa mkataba wa miaka mitatu na Shirika la Bima la Taifa (NIC) wenye thamani ya Sh. milioni 900 kwa ajili ya tuzo hizo za mchezaji bora wa timu.**

Rais wa klabu hiyo, Hersi Said, akizungumza jijini Dar es Salaam jana alisema mkataba huo utakuwa unalenga moja kwa moja kwa mchezaji bora wa kila mwezi.

"Tutahakikisha mkataba utawapa thamani sahihi ya kile walichokiwekeza kwetu, mkataba huu ni heshima kubwa kwa Yanga.

"Kufanya kazi na kampuni kubwa kama hii ni kutokana na utendaji wetu sahihi ndani ya klabu yetu, tunawahakikishia ushirikiano mkubwa sana kutoka kwetu na tutakwenda mbali zaidi ya hapa sisi na Kampuni ya NIC," alisema Hersi.

Katika hatua nyingine, kuelekea mchezo wao ujao wa Ligi Kuu Bara, Azam FC imemrudisha darasani Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, akianza kazi ya kuifuatilia na kusoma ubora na udhaifu ili kuufanyia kazi kuhakikisha wanavuna alama tatu muhimu watakapokutana hapo Oktoba 25, mwaka huu.

Ligi Kuu Bara kwa sasa imesimama hadi Oktoba 23, mwaka huu, kupisha Kalenda ya Fifa na siku mbili baada ya kuporejea Yanga itakuwa na shughuli pevu dhidi ya Azam FC.

Akizungumza na Nipashe jana, Gamondi alisema amepata muda wa kuangalia mechi za Azam FC na ameona ubora wa kikosi cha wapinzani wao hao, hivyo atahakikisha wanazifanyia kazi katika uwanja wa mazoezi.

Alisema anaimani haitakuwa mechi rahisi kwa sababu kila mmoja anahitaji kupata alama katika mchezo huo ukizingatia wamepoteza mechi dhidi ya Ihefu FC.

"Tunatambua wapinzani wetu ni imara, nasi tutafanya kazi kutafuta ushindi kwenye mechi hiyo, hilo tunalitambua tutacheza kwa umakini ushindi ndio kuwafurahisha mashabiki wetu.

"Wachezaji wanatambua umuhimu wa kila mechi na wapo tayari kuona tunapata ushindi na kufanyia kazi makosa kwenye mechi zilizopita ili kuwa bora na imara zaidi kuelekea mchezo wetu huo," alisema kocha huyo.

## Chama ajitabiria kiatu ufungaji bora Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Simba, Clatous Chama, ameeleza kufurahishwa kwake kuanza ligi kwa kufunga mabao kwenye viwanja vya mikoani kitu ambacho misimu ya nyuma kilikuwa kigumu mno kwake, akitabiri anaweza kuwa na mabao mengi zaidi msimu huu kuliko wakati mwingine wowote tangu acheze soka nchini.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mzambia huyo alisema wakati timu yake ya Simba ikipata ushindi mara tatu mfululizo kwenye viwanja vya ugenini, na yeye ameshafunga mabao mawili kitu ambacho hajawahi kukifanya tangu atue nchini.

"Kusema ukweli nimefurahi sana, kwa misimu mingine tangu nicheze soka hapa Tanzania nimekuwa nikipata shida sana kufunga mabao kwenye hivi viwanja vya mikoani kwani kuna wakati vinakuwa havipo katika hali nzuri, lakini mpaka hii raundi ya tano nimefunga mabao mawili ugenini," alisema.



Chama alifunga bao la kwanza, Agosti 17 kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Simba ikiichapa Mtibwa Sugar mabao 4-2 na Alhamisi iliyopita alipachika bao la pili msimu huu kwenye Uwanja wa Sokoine, jijini Mbeya, akiiongoza timu yake kushinda 3-1 dhidi ya Prisons.

Mabao yote hayo aliwafunga kwa kutumia mguu wa kushoto.

Chama alisema kama ameanza kufunga kwenye viwanja vya mikoani ambavyo vilikuwa vigumu kwake, anaweza kufunga mabao mengi msimu huu pale Uwanja wa Benjamin Mkapa utakapofunguliwa.

INAENDELEA UKURASA 23



9 770856 541002 >